epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Machi 22, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581623
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

## BAYERN YATOA OFA YA MWISHO KWA DAVIES



**Utata** dereva gari la watalii kufa mikononi mwa polisi

UKURASA 2

**TANAPA** yajivunia ongezeko wageni, yatangaza aina mpya ya utalii



UKURASA 4

**Leseni** kubwa ya kuchimba madini ya tembo yatolewa

UKURASA 7

## 'Kombi' mpya za kidato V & VI zagawa wadau

UKURASA 4

# Dk. Mpango: Nitajiuzulu

- **Atishia** kuchukua uamuzi huo iwapo...

*Endelea ukurasa 2*



Mwonekano wa maendeleo ya ujenzi wa mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe, katika eneo la Nyumba ya Mungu, wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro, uliokaguliwa jana na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (picha ndogo). **PICHA: OMR**



Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni

# Vigogo 14 kizimbani mashtaka uhujumu bil. 2/-, yumo DED

UKURASA 7

**MICHEZO** PRODUCER WA DITTO ATOA USHAHIDI MAHAKAMANI UK.24 **KATUNI** UK.6

# Mwanafunzi alawitiwa akitoka kuchukua notisi kwa rafiki yake

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

MWANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Mkolani, mkazi wa kata ya Mkolani (mtaa tunauhifadhi), jijini Mwanza, amedaiwa kulawitiwa na vijana wanaotajwa kutoka mtaani kwao wakati akitoka kwa rafiki yake kutafuta notisi kwa ajili ya kujisomea.

Ni ukatili unaodaiwa kutendwa Februari 18, mwaka huu, mama wa mtoto huyo akidai kukosa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika kuwasaka wahalifu hao. Anadai polisi wamemtaka awatafute mwenyewe na kutoa taarifa kwao pindi atakapowapata.

Akisimulia tukio hilo juzi, mwanafunzi huyo (mvulana mwenye umri wa miaka 16), alidai kufanyiwa ukatili huo wakati akienda kwa rafiki yake kuchukua daftari la notisi, njiani alikutana na watu hao, wakamtenda ukatili huo huku wakimtishia kumuua ikiwa atatoa taarifa za tukio hilo.

"Waliniziba mdomo na kunivua nguo kisha wakanilawiti na baada ya kunilawiti wakanipiga fimbo na wakanitishia kuniua pindi nitakapojaribu kutoa taarifa hizi nyumbani au kwa mtu yeyote.

"Baada ya hapo wakaniachia, nikaondoka huku nikihisi maumivu makali. Nilipofika nyumbani, kaka yangu akaniuliza, nikamuelezea na mama alivyokuja tukamwambia," alisimulia mwanafunzi huyo.

Mtoto huyo alisema kwa sasa anaogopa kutoka nje ya nyumba yao na hata kwenda shuleni kwa sababu ya vitisho alivyopewa na watu hao aliodai kuwa anawafahamu.

Alidai kuwa taarifa kuhusu vijana hao wameshazifikisha kituo cha polisi, lakini hawajachukuliwa hatua ingawa mmojawao alikamatwa na polisi na baadaye kuachiwa kwa dhamana.

Mama mzazi wa mwanafunzi huyo (jina tunalo) alisema kuwa baada ya kupewa taarifa hizo, alimpigia simu Mwenyekiti wa Mtaa ambaye alimtaka atoe taarifa kituo cha polisi na alipofika na kutoa maelezo polisi, alipewa RB pamoja na Fomu Namba Tatu ya Polisi (PF3) kwa ajili ya matibabu ya mtoto.

Alisema kuwa baada ya kumpeleka mwanawe Hospitali ya Butimba na kufanyiwa vipimo, ilithibitika alilawitiwa na ndipo taratibu za matibabu zilifuata na baadaye waliruhusiwa kurudi nyumbani.

"Wahusika hawajachukuliwa hatua mpaka sasa, maana awali niliambiwa niwatafute, nikiwapata nitoe taarifa polisi. Sasa mimi ninawatafutaje? Hilo ni jukumu langu? Tulifanikiwa kumpata mmoja wa (wanaodaiwa) wahalifu walioshiriki tukio hilo, lakini alikamatwa lakini amepewa dhamana na sasa yupo hapa mtaani," alidai mama huyo.

Mmoja wa wakazi wa kata hiyo, Selestine Wilbard alisema hakuna maana ya kuwa na polisi ilhali waliotendwa uhalifu wanatakiwa wao wawatafute wahalifu.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Gidion Msuya, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia ukatili huo, alisema kijana huyo alikwenda kituo cha polisi na kuhudumiwa.

Alisema kuwa baadaye alikamatwa kijana aliyedaiwa kuwa mmoja wa wahusika kwenye tukio hilo, lakini alipoitwa mtendwa kufanya utambuzi, alisema kijana aliyekamatwa hakumlawiti, hivyo akaachiwa kwa dhamana na anaendelea kuripoti kituoni na jeshi hilo linaendelea na uchunguzi kuwapata vijana hao.

Vilevile, alisema ushirikiano wa jamii kwa polisi kufichua vitendo hivyo ni mdogo, hivyo kufanya kazi ya ufuatiliaji matukio hayo kuwa ngumu.

"Wanatakiwa kuleta taarifa dhania kwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya (OC-CID) na kutuambia tu ni yule, sisi tutawakamata lakini pia kuna sheria ya wananchi wenyewe kukamata, lakini kwa kesi kubwa kama hizo watuoneshe tu ni hawa, tutawakamata, wala hakuna mambo ya kuvutana," alisema Kamanda Msuya.

Ni kosa la jinai kumwingilia kinyume cha maumbile mwanamke au mwanamume na adhabu yake ni kifungo cha miaka 14 gerezani kwa mujibu wa kifungu cha 290 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16.

Kwa kuwa aliyetendwa ukatili huo ni mtoto, wahusika wanaweza pia kuadhibiwa kutumikia kifungo cha maisha gerezani kwa mujibu wa Kifungu cha 131A(2) kinachokataza kubaka mkiwa katika kikundi.

# Dk. Mpango atishia kujiuzulu

**Na Mary Mosha,** MWANGA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema yuko tayari kujiuzulu wadhifa wake, endapo mradi mkubwa wa Maji wa Mwanga/Same/Korogwe unaotarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wananchi 438,000 hautakamilika kufikia Juni, mwaka huu.

Mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 300, unafadhiliwa na serikali ya Tanzania, kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa na mashirika ya misaada ya kimataifa kutoka nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo jana alipotembelea na kukagua mradi huo katika kijiji cha Kiria, Mwanga mkoani Kilimanjaro.

"Sina uso wa kuja kuwatazama wananchi hawa walioahidiwa upatikanaji wa maji kwa miaka 19 iliyopita. Mimi nitajiuzulu ila sijui nini kitatokea kwa walioko chini yangu, hasa Waziri wa Maji na waliko chini yake.

"Viongozi wa wizara, mradi huu uwe eneo lenu la kudumu. Hakikisheni maji haya yanapatikana. Ikiwa kuna changamoto zitatueni kabla. Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro (Nurdin Babu) kwa kusaidiana na walioko chini yako, pangeni ziara za kutosha hapa; nami nitakuja kabla ya muda huo hapa," alisema.

Katika maelekezo yake, Dk. Mpango alimkumbusha Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mwajuma Waziri, wakati wa kiapo chake kushika wadhifa huo, Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa maelekezo kwa wizara hiyo kwamba ifikapo Juni, mwaka huu, maji yapatikane Same na Mwanga (Kilimanjaro) na Korogwe (Tanga).

"Nafikiri ulisikia 'very clear' (kwa ufasaha). Jana nilikuwa naongea na Waziri wa Maji (Jumaa Aweso); nataka nirudie tena mjipange vizuri. Wasimamieni makandarasi, bahati nzuri mmesema hapa wana uwezo, usiku na mchana maji yatoke mwezi Juni.

"Mradi huu umekuwa kero kwa wananchi wa maeneo haya. Wewe hesabu kuanzia 2014 wakati umeanza kutekelezwa. Pangeni zamu za kuja hapa usiku na mchana. Wekeni kempu (kambi) hapa," alisisitiza.

Mradi huo unatekelezwa kwa gharama zinazojumuisha ufadhili wa Benki ya Kiarabu inayosimamia Maendeleo ya Nchi za Afrika (BADEA), Mfuko wa OFD unaojumuisha nchi zinazozalisha mafuta (OPEC) na Mfuko wa Maendeleo wa Kimataifa wa Saudi (Saudi Fund) na Mfuko wa Misaada wa Kuwait (Kuwait Fund).

Akitoa maelezo kuhusu maendeleo ya mradi huo, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mwajuma Waziri, alisema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 85.7 na utakamilika Juni, mwaka huu, kama ilivyopangwa.

"Mradi unatarajiwa kuzalisha kiasi cha lita za ujazo milioni 103,650 kwa siku na tunaamini kwamba utafikia kiwango chake cha kukidhi mahitaji ya wananchi wa eneo la mradi hadi kufikia mwaka 2038," alisema Mwajuma.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizindua Miongozo Saba ya Kisheria, wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali wa Tanzania, jijini Dodoma jana, wenye kaulimbiu ya "Upatikanaji wa Huduma za Kisheria kwa Wananchi ni Nguzo Muhimu kwa Ustawi wa Jamii". Kulia ni Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Felishi. **PICHA: OWM**

# Utata waibuka dereva gari la watalii kufa mikononi mwa polisi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

UTATA umeibuka kuhusu mazingira ya kifo cha dereva wa gari maalum la kubeba watalii, Omari Msami (48), uchunguzi umeanza ukihusisha wataalamu wa uchunguzi wa vifo, ndugu na Jeshi la Polisi.

Msami, mkazi wa Philips, jijini Arusha, anadaiwa kupoteza maisha akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi wilayani Karatu, mkoani Arusha Machi 16, mwaka huu.

Kaka wa marehemu, Hamidu Maftaa, alidai jana jijini hapa kuwa mdogo wake Omari, aliyekuwa dereva wa kampuni binafsi ya utalii, siku ya tukio alisimamishwa na askari hao na kushindwa kuelewana.

Inadaiwa dereva huyo alisimamishwa na askari wa doria katika kizuizi cha Manyara-Kibaoni kilichoko Wilaya ya Karatu, lakini hakukuwa na maelewano kati ya dereva huyo na askari wa doria.

"Baada ya kushindwa kuelewana na marehemu, inadaiwa kwamba askari hao waliamua kuendesha gari hilo la watalii wakiwa wamembeba ndani yake na kumpeleka hadi Kituo cha Polisi Karatu kisha baadaye kumpeleka Hospitali ya Wilaya hiyo.

"Hatujui kama ndugu yetu alifikwa na umauti akiwa eneo la tukio, njiani au hospitalini, ndio maana tunataka haki itendeke, ili ukweli wa tukio hilo ujulikane na wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Kutokana na utata huo, juzi Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna wa Polisi, David Misime, kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari, alisema:

"Tukio la kifo cha Omari Saimon Msami, ambaye taarifa zake zimeonekana kusambaa katika baadhi ya mitandao ya kijamii, lilitokea Karatu, mkoani Arusha. Lilianza kufanyiwa uchunguzi tangu liliporipotiwa kutokea Machi 16, 2024.

"Kutokana na mazingira ya tukio hilo yalivyo, Jeshi la Polisi limeona umuhimu wa kushirikisha wataalamu mbalimbali, hasa wanaochunguza matukio ya vifo na baadhi ya ndugu kulingana na uhitaji wa uchunguzi."

Alisema imebidi kufanya hivyo kutokana na mtiririko wa maeneo aliyotembelea baada ya kuwarudisha wageni wake maeneo waliotakiwa kulala jioni ya Machi 15, 2024.

Kwa mujibu wa Naibu Kamishna Misime, uchunguzi unaofanywa na wataalamu utakapokamilika na ushahidi ukibainisha kifo kimesababishwa na mtu yeyote yule, hatua za kisheria zitachukuliwa bila kujali cheo chake na nafasi yake katika jamii.

Akiwa katika maombolezo ya kifo hicho cha mwanawe nyumbani kwake, mama mzazi wa marehemu Omari, Janeth Kamugisha, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati jambo hilo ili kupatikana alichokiita "haki ya mwanangu".

"Mwanagu ameuawa kikatili. Rais Samia upo wapi? nisaidie, unajua uchungu wa mwana. Ameniachia watoto wadogo watatu na mjane. Nani atawalea?

"Tunataka serikali iwalee. Hawa waliomuua hawajakamatwa, nisaidie Rais Samia," alitamka mama huyo huku akilia.

TANGAZO


Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jambo Kubwa
Linakuja
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com



Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Kinywa, Ekaristo Mwang'ande (kushoto) akimpatia matibabu Naibu Makamu Mkuu Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Prof. Emmanuel Balandya, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Afya ya Kinywa na Meno Duniani katika Shule ya Meno Muhimbili (MUHAS - SoD), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TANAPA yajivunia ongezeko wageni, yaja na utalii mpya

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa nchini (TANAPA) limesema idadi ya watalii watakaotembelea hifadhi za taifa itaongezeka hadi kufikia milioni tano mwakani.

Hayo yalisemwa jana na Kamishna Mkuu wa TANAPA, Musa Kuji, katika kikao kazi na waandishi wa habari na wahariri kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana chini ya uratibu wa Ofisi ya Msajili nchini.

Kuji alisema, kuongezeka kwa idadi hiyo ya watalii watakaotembelea hifadhi hizo ni mwendelezo wa mafanikio ambayo shirika hilo linaendelea kuyapata kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita kuanzia mwaka 2021 hadi 2024.

"Mafanikio haya nitakayoyaeleza leo hii msingi wake mkuu ni jitihada za makusudi zinazoendelea kufanywa na Dk. Samia Suluhu Hassan, ambazo zinaambatana na ushiriki wake wa moja kwa moja kwenye kukuza sekta ya uhifadhi wa wanyamapori na utalii ikiwamo kwenye filamu maarufu ijulikanayo kama "Tanzania: The Royal Tour.

Alisema mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na; kukuza na kuendeleza utalii baada ya filamu hiyo kufungua milango ya utalii na fursa za uwekezaji katika hifadhi hizo hasa baada ya nchi kutoka kwenye athari za janga la UVIKO-19.

Kwa mujibu wa Kuji, mwaka 2018/19 watalii waliotembelea hifadhi hizo walikuwa 1,452,345 wakiwamo wa ndani 719,172 na nje 733,173.

"Vivutio vyetu kupitia filamu ya "Tanzania: The Royal Tour" mwaka 2021/2022 idadi ya watalii ilianza kupanda na kufikia 997,873," alisema.

Alisema idadi hiyo iliendelea kupanda, mwaka 2022/23, watalii waliongezeka hadi kufikia 1,670,437.

Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka jana hadi Machi 19, mwaka huu, watalii 1,514,726, wa ndani 721,543 na wa nje 793,183 walitembelea hifadhi hizo.

Alisema idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia tano ikiwa ni zaidi ya lengo la kupokea watalii 1,387,987 (wa nje 827,713 na watalii ndani 726,676 katika kipindi hicho.

Idadi ya watalii wanaotarajiwa kutembelea Hifadhi za Taifa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni 1,830,081 wa nje 963,413 na ndani 866,667.

"Ongezeko la watalii kukaa nchini limechangia mapato kutoka Sh. 174,715,158,494 (2021/22) hadi Sh. 337,424,076,896 (2022/23) sawa na ongezeko la Sh. 162,708,918,402 (sawa 94%).

Alisema katika mwaka wa fedha 2023/24 (Julai 2023 hadi Machi 19, 2024) TANAPA imekusanya Sh. 340,101,108,465 ikilinganishwa na matarajio ya kukusanya Sh. 295,466,811,506 hadi mwezi huu.

Alitaja mafanikio mengine ni kuongezeka kwa masoko mapya ya utalii kutembelea hifadhi hizo ikiwa ni pamoja na nchi za China, Urusi, Ukraine, Poland, Jamhuri ya Czech na Israeli.

TANAPA imeendelea kupata tuzo zinazotolewa na taasisi ya ESQR kwa kipindi cha miaka minne mfululizo, kati ya hizo za miaka mitatu.

Hifadhi ya Taifa Tarangire na Kilimanjaro zilipata tuzo mara mbili mfululizo kwa mwaka 2021 na 2022 ya kuwa vituo vyenye mvuto katika utalii (best of the best outdoor enthusiasts). Tuzo hizi hutolewa na jukwaa la kimataifa lijulikanalo kwa jina la "Trip Advisor". Pia, kampuni ya Explore Worldwide yenye makao yake makuu nchini Uingereza, mwaka huu 2024 imeutambua Mlima Kilimanjaro kuwa namba moja ya alama za asili za kudumu na zinazokumbukwa zaidi ulimwenguni (World's topmost unforgettable natural landmarks).

TANAPA inasimamia Hifadhi za Taifa 21 zenye eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 96,908.88 ambalo ni sawa na asilimia 10.2 ya eneo lote nchini.

# 'Kombi' mpya wanafunzi wa kidato V & VI zagawa wadau

**Na Waandishi Wetu**

WADAU wa elimu nchini wamekuwa na mtazamo tofauti kuhusu tahasusi ('kombi') mpya 49 zilizotangazwa juzi na serikali, huku sekta binafsi wakitaka ushirikishwaji.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti jana ni pamoja na Richard Mabala ambaye alipongeza serikali kwa kuja na tahasusi hizo mpya, lakini akawa na angalizo kwamba kuna haja kushirikisha wadau binafsi ili kuongeza tija katika ufundishaji.

Alisema maandalizi yanahitajika hususan katika eneo la ujifunzaji kwa kuwapo walimu na vitabu vitakavyokidhi mahitaji mapya ya tahasusi hizo mpya, akishauri waandishi binafsi wapewe fursa ya kuandika vitabu.

"Walimu wapo wa hizi tahasusi zote? Vitabu vimeandaliwa kwa hizi tahasusi zote? Inabidi Taasisi ya Elimu iandike vitabu vipya, kweli wameweza kuandaa vitabu?

"Maoni yangu ni kwamba, ninatamani wangekuwa wametuambia hayo, tujadili na tahasusi zianze mwaka kesho baada ya maandalizi ya kutosheleza, kuna maoni mengi ya wananchi wanatoa, na mimi ninayaona," alisema Mabala.

Alisema kuwapo tahasusi za lugha kama vile Kiarabu na Kichina ni kati ya zilizo kubwa duniani, kutaongeza wigo wa watanzania kujifunza zaidi.

"Kwani kuna ulazima wa kujifunza lugha za Ulaya tu? China wanatawala sana kiuchumi, wapo wengi sana hapa na hata kwa majirani zetu. Kwa kaskazini mwa bara letu, watu wanaongea Kiarabu na Waarabu uchumi wao mzuri, sioni ubaya," alifafanua.

Mabala aliongeza: "Baiolojia kuunganishwa na 'Nutrition na Food' sioni ubaya, ila zingine ninashindwa kuelewa uhusiano wake, ile ya ushonaji hasa.

"Kwa kuwa wameanzisha hizi tahasusi zote, kwanini taasisi ya elimu iendelee kuwa na ukiritimba wa kuandika vitabu? Kwanini wasipewe wachapishaji na watu binafsi wengine waandike?

Alisema inapotolewa fursa kwa wadau wa elimu kuandika na kuchapisha, idadi ya tahasusi mpya inaendana na kuwapo vitabu.

Tahasusi mpya zitakazoanza kutekelezwa Julai, mwaka huu, zipo katika makundi saba ambayo ni: Tahasusi za Sayansi ya Jamii; Tahasusi za Lugha; Tahasusi za Masomo ya Biashara; Tahasusi za Sayansi; Tahasusi za Michezo; Tahasusi za Sanaa; na Tahasusi za Elimu ya Dini.

Suzan Lyimo, mbunge mstaafu na mdau wa elimu, aliunga mkono uamuzi huo wa serikali, akisema itakuwa rahisi kwa wanafunzi kufanya chaguo la tahsusi, matokeo ya mitihani yakishatoka.

"Kuongeza tahsusi kutoka 16 hadi 65 ni hatua nzuri kwani tunafuata soko la ajira, watu kujiajiri wenyewe. Kwa mfano uchoraji, mambo ya kutengeneza nguo, vijana wakiwa na ujuzi huo wanaweza kutumika katika viwanda vya nguo kuweka picha katika kanga au kitenge na kazi nyingine zinazohusika na uchoraji," alisema Suzan.

Kwa upande wa lugha, Suzan alifafanua kuwa Tanzania si kisiwa; ni muhimu Watanzania wawasiliane na wenzao katika nchi mbalimbali duniani, hivyo ni muhimu kujua lugha za kimataifa.

Pamoja na pongezi, Suzan ana angalizo kwamba hatua hiyo ya serikali huenda isiwe na matokeo chanya kwa kuwa haina walimu wa kutosha wa fani mbalimbali zinazohusu masomo hayo.

"Je, tuna walimu wa kutosha wa sekondari, vyuo vikuu na viwanja vya kutosha vya mambo ya sanaa na michezo? Pamoja na kwamba nimepongeza uamuzi wa serikali, lakini sina uhakika kama kuna wataalamu hao wa kutosha nchini," alisema.

Katibu wa Chama cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu (CHAKAMATWA), Meshack Kapange, alisema inachokifanya serikali ni jambo jema, lakini inakwepa gharama ya maandalizi kwa kuruka baadhi ya hatua. Ni kuvuruga utaratibu wa elimu nchini.

Alisema serikali imeleta tahasusi hizo, lakini hakuna walimu wa kutosha walioandaliwa kwa ajili ya kufundisha masomo husika, hata masomo ya awali hayana walimu wanaotosheleza.

Kapange alisema elimu ya nchini imechanganywa na siasa na kwamba tahasusi zilizoongezwa si mpya bali zilikuwapo, lakini zikaachwa.

"Hawa watu wanachezea elimu, leo kwenye mtaala wanasema kuna tunu za taifa, bado kwenye katiba hatujazitambua mnazipelekaje shuleni?

"Wanachezea elimu ya watoto wetu kwani inatakiwa ishirikishe wadau wote. Wamepeleka masomo ya amali, tuna walimu wa kutosha?

"Waziri anasema kutakuwa na mawakala wa Vyuo vya Ufundi (VETA) kila mahali, hao kiuhalisia hawajasomea ualimu, wamesomea ufundi tu, hawana maadili ya ualimu na hawajui jinsi ya kukuza vizazi, huwezi kwenda kufanya marekebisho bila kuwa na nguvukazi ya kutosha ya walimu na vifaa vya kufundishia," alitahadharisha.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale, Joyce Lameck, Maulid Mmbaga na Sabato Kasika.**

**MIAKA MITATU YA MHE.RAIS DK.SAMIA SULUHU HASSAN NA UTEKELEZAJI.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI TABORA (TUWASA)

# Bil.149 zilivyoleta neema upatikanaji Maji TABORA miaka mitatu ya Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

Katika kipindi cha miaka mitatu ya utawala wa Mhe.Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (2021-2024) Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Tabora (TUWASA) imepokea zaidi ya Sh.bilioni 4.6 kutoka serikali kuu pamoja na Dola za Kimarekani 62,287,420 sawa na zaidi ya Sh.bilioni 145 kutoka India na kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya Maji mkoani hapa.

Kupitia fedha hizo TUWASA imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali kwenye sekta ya maji mkoani hapa ambayo ilikuwa katika malengo na mipango ya Mamlaka hiyo kwa kipindi cha miaka mitano.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa TUWASA Mhandisi Mayunga Kashilimu anasema Mamlaka hiyo ililenga Kuboresha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waliokuwa mbali na mtandao wa bomba kuu katika Manispaa ya Tabora maeneo ya Kidatu A, Kidatu B, Ikindwa, Mawiti, Chang'ombe, Mtakuja, Ulamba, Misha Utusini na Misha Ufugajini.

Lakini kupitia fedha zilizotolewa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassani kupitia Mpango wa Utekelezaji Miradi kwa Fedha za UVIKO-19 wamefanikiwa kutumia zaidi ya Sh.milioni 547 kwaajili ya kulaza mtandao wa bomba zenye urefu wa kilomita 42.055,Kuunganisha jumla ya kaya 1,000 kwenye huduma ya maji pamoja na kujenzi wa vituo vinne vya kutekea maji ambako hatua hizo zimekamilika kwa asilimia 100.

Vilevile imefanikiwa katika ujenzi wa mradi wa maji kwa matokeo ya haraka (QUICKWIN) katika Kata za Ntalikwa, Tumbi, Ikomwa na Kakola uliogharimu zaidi ya Sh.milioni 601 kwa kulaza bomba kwa urefu wa km. 23.164, kuunganisha vituo 10 vya kutekea maji ambako utekelezaji wake umefikia asilimia 75.



Mhe. Dk. Rais Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Aidha fedha hizo zilizotolewa zilifanikisha ujenzi wa mradi wa maji kwa matokeo ya haraka katika mji wa Sikonge uliogharimu zaidi ya Sh.milioni 484 na umekamilika kwa asilimia 100 kwa kulaza mtandao wa bomba zenye urefu wa kilomita 28.164,kuunganisha jumla ya kaya 150 kwenye huduma ya maji na Ujenzi wa kituo kimoja cha kutekea maji.

Kupitia miradi hiyohiyo ya matokeo ya haraka TUWASA imefanikiwa kulaza bomba urefu wa km 14.377,Ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ukubwa wa lita 50,000 ,Kuunganisha jumla ya kaya 110 kwenye huduma ya majiambako zimetumika zaidi ya Sh.milioni 503 na tayari ujenzi umekamilika kwa asilimia 100.

Pia kupia fedha hizo zaidi ya Sh.milioni 287 zimefanikisha ujenzi kwa asilimia 100 wa Maji katika mji wa Isikizya kwa kulaza bomba urefu wa km 14.377 pamoja na kuunganisha jumla ya kaya 80 kwenye huduma ya maji.

Pia Mhe.Rais Samia kupitia fedha hizo amesaidia kuboresha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waliokuwa mbali na mtandao wa bomba kuu katika Manispaa ya Tabora maeneo ya Kata za Ikomwa, Uyui, Kakola, Kabila (Umanda-Igosha) na Ndevelwa.Katika maeneo hayo TUWASA imefanika kulaza mtandao wa bomba zenye urefu wa kilomita 30,kuunganisha jumla ya vituo 16 vya kutekea maji.

TUWASA inaendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa bwawa la kutibu majitaka katika Manispaa ya Tabora Ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka (Construction of Sludge Facility),Ununuzi wa gari moja ya kunyonyea majitaka lenye ukubwa wa Lita 6,000(6.0 m3) ambavyoo vyote kwa pamoja vinagharimu zaidi ya Sh.bilioni 1.6 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 40 chini ya fedha kutoka serikali kuu.

Kuhusu Dola za Kimarekani 62,287,420 sawa na fedha za kitanzania Bilioni 145 kutoka EXIM Bank India zinatumika katika utekelezaji wa Mradi wa maji wa miji 28 katika maeneo ya Sikonge, Urambo na Kaliua ambapo mpaka upo asilimia 34 kwa Ulazaji wa bomba kuu za usafirishaji na usambazaji wa maji na Ujenzi wa matenki ya kuhifadhia maji maeneo ya Sikonge, Urambo na Kaliua.

Mkurugenzi Mtendaji wa TUWASA Mhandisi Mayunga Kashilimu anasema Katika miaka mitano ijayo, TUWASA inalenga kuhakikisha kaya nyingi mijini zinaunganishwa katika mtandao wa majitaka sambamba na kuona nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2025.







Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la mchakamchaka wanafunzi liungwe mkono

**MAGONJWA** kama maradhi ya moyo, shinikizo la juu la damu, figo na kisukari, yamekuwa yakiongezeka kila mwaka, hivyo kusababisha watu wengi kupoteza maisha. Sababu kubwa ambayo imekuwa ikitolewa na wataalamu wa afya ni mtindo wa maisha kutokana na watu kula vyakula vyenye wanga na mafuta kwa wingi, unywaji wa pombe uliopitiliza na kutokufanya mazoezi.

Hali hiyo ya ujumla inatokana na mtindo wa maisha kwa sababu watu wamekuwa wakitumia muda mwingi kukaa kwenye viti ofisini au nyumbani bila kujishughulisha na kazi za kuwafanya hata kutoa jasho.

Mtu anayefanya kazi ofisini, kwa mfano, akitoka nyumbani anaingia kwenye gari hadi kazini na akifika atatumia saa nane au zaidi akiwa amekaa kwenye kiti. Akishamaliza kazi, atapanda gari hadi nyumbani na baada ya kufika, atakaa kwenye kiti akipumzika na baadaye kula chakula kisha kwenda kitandani.

Hata watoto, hususan wanaosoma shule za mchepuo wa Kiingereza, ambazo wazazi wenye uwezo wa kati na wa juu kiuchumi wanaziona ndizo bora kwa elimu yao , wamekuwa na mfumo wa namna hiyo. Watoto wanachukuliwa asubuhi kwa magari kutoka nyumbani kwenda shuleni na kisha kurudishwa wakiwa kwenye mabasi ya shule.

Huo ndio mfumo mzima wa maisha wa miaka mingi kwa watu wengi hasa waishio kwenye miji mbalimbali. Matokeo yake watu wamekuwa wanakumbwa na maradhi ambayo yanasababisha afya kuzorota na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya matibabu na baadhi kupoteza maisha.

Kutokana na kasi ya kuenea kwa maradhi hayo ambayo huathiri kwa kiasi kikubwa nguvu kazi ya taifa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ameibuka na wazo ambalo amelifanya kuwa agizo kwa wanafunzi wa shule zote mkoani humo kuanza kukimbia mchakamchaka kabla ya kuanza masomo ili kuwaweka katika hali nzuri ya kiafya. Pia alisema hali hiyo itawafanya vijana kuwa na afya, ukakamavu na uzalendo hatimaye kuwaepusha na maradhi yasiyo ya kuambukiza.

Akitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Wadau wa Elimu mapema wiki hii, mkuu huyo wa mkoa alibainisha kwamba hakuna mwanafunzi anayeweza kufanya vizuri kwenye masomo kama hayuko vizuri kiafya. Ili kumfanya awe timamu katika afya na hatimaye kufanya vizuri katika masomo, mkuu huyo wa mkoa alisisitiza kuwa mazoezi ndiyo njia pekee.

Sambamba na kuwa katika afya njema, Senyamule alisema mchakamchaka utawafanya wanafunzi kuwa wazalendo pia kutokana na nyimbo watakazokuwa wanaziimba kwenye mazoezi hayo ya kuchangamsha mwili ili kuwaweka timamu kiafya na kufanya vizuri katika masomo.

Kwa hakika jambo hilo limeungwa mkono na baadhi ya wakazi wa mkoa wa Dodoma waliohojiwa na gazeti hili kwamba hali hiyo itawawezesha vijana kuwa wakakamavu na kuamsha ari ya kujitambua na kufanya mambo mazuri kimaisha, ikiwamo masomo.

Kitendo cha kubuni na kuagiza wanafunzi wakimbie mchakamchaka asubuhi kabla ya masomo ni cha kupongezwa na kinaonyesha kiongozi huyo kuwa mbunifu na mwenye kutambua wajibu wake na anayeangalia mambo kwa mawanda mapana.

Ni ukweli ulio wazi kwamba afya ni suala la msingi katika maisha ya mwanadamu kwa kuwa mtu akiwa timamu kimwili, ana uwezo wa kufanya mambo vizuri tofauti na yule ambaye hayuko vizuri katika eneo hilo. Matokeo yake, hata hali za kimaisha baina ya watu hao ni lazima zitakuwa tofauti.

Mchakamchaka ulikuwa jambo la msingi kabla ya miaka ya 2000 kwa kuwa ilikuwa lazima kila mwanafunzi mwenye utimamu wa mwili akimbie na aliyeshindwa kufanya hivyo alichukuliwa hatua ama kwa kuchapwa viboko au kupewa adhabu ya kufanya usafi kwa muda fulani.


Hata afya za wanafunzi kwa wakati huo zilikuwa imara na kizazi hicho kilijitambua tofauti na sasa. Kongole RC Senyamule, viongozi wengine waige jambo hilo kwa manufaa ya afya za nguvu kazi ijayo ya Watanzania.

•Maoni haya yamerudiwa kwa sasabu za kiufundi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tufuge wanyama, ila tuwe makini na hatari zaidi kiafya

Na Tuntule Swebe

**UKWELI** ulioko jamii yetu sasa ina vitu vingi vinavyoizunguka, mfano miti, majani na vyanzo vya maji. Katika yote hayo, ni vyanzo vizuri vinavyomuwezesha mwanadamu kuishi mahali tulivu na pakupendeza

Kwa upande wa pili, binadamu kwa kiasi kikubwa cha maisha yake kimetawaliwa na wanyama, kwani viumbe hai ni sehemu ya furaha katika maisha ya watu wengi kama vile mbwa, paka, ng,ombe, kondoo, nguruwe, mbuzi na kadhalika.

Wanyama hao hutumika kama sehemu ya kuondoa mawazo kwa watu wengi, wakipata faraja.

Tunapowazungumzia mbuzi, nguruwe, kondoo, ng'ombe, hapo watu wengi hujipatia pesa kwa kuuza maziwa na nyama.

Wakati mwingine, watu hao huuza nyama hao wakidumu kuwa sehemu ya biashara zao, kwani wapo wengine wamefungua bucha za nyama. Hivyo, walio wengi wamenufaika kupitia wanyama na maisha yao wakijikita na ufugaji huo.

Niwahamasishe, wasisite milango ipo wazi isipokuwa wakumbuke cha kuzingatia, ili kuepuka magonjwa ya wanyama

Nilipata kuona taarifa ya chombo kimoja cha habari cha kimataifa, kikitufahamisha upande wa pili wa shilingi, nyama ya nguruwe ina madhara, ilhali hapa kwetu ina umaarufu katika hata kuwa na majina mengi kama vile 'mkuu wa meza' na 'kitimoto'.

Hata hivyo, utafiti wa kisayansi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Morogoro umebaini kuwa walaji wengi wanyama ya nguruwe wapo hatarini kupata magonjwa kama vile kifafa, kutokana na minyoo tegu iliyopo kwenye nyama ya mnyama huyo.

Amenukuliwa Mtafiti wa Magonjwa ya Binadamu na Wanyama, Dk. Mathias Emmanuel kutoka chuoni SUA, anashauri ingefaa zaidi, kama wanyama hao wangeliwa kwa tahadhari za kiafya.

Mwaka jana kulitajwa kuwapo magonjwa 200 yanayohusishwa nayo, kati yake kuna magonjwa yanayoathiri watu kama vile kichaa cha mbwa.

Kimsingi, binadamu anaweza kupata kichaa cha mbwa kwa kuumwa na mnyama aliyeathirika na virusi hivyo na mtu kupata maambukizi ya ugonjwa huo. wanyama wanoweza kuambukiza ugonjwa huo ni mbwa, paka na fisi.

Mtu unapokuwa karibu na paka, unatakiwa kuwa makini kuhakikisha asikuparue na makucha yake, kwani anapokukwaruza, unaweza kuaambukizwa maradhi hayo yanayosababisha bakteria kumuingilia mtu.

Ni ugonjwa wenye dalili za kuumwa kichwa, uchovu, homa kwa mujibu wa kituo komja cha afya nchini Marekani.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abbdallah Ulega, anawataka wataalamu wa afya za binadamu na wanyama, kujenga mkakati na nyendo za kukabili ongezeko la usugu wa vimelea na matumizi mabaya ya dawa.

Anasema asilimia70 ya magonjwa ya binadamu yanatokana na wanyama. Mojawapo ni yanayowakabili watu ni ugonjwa wa 'wasiwasi' ambao huwapata zaidi wajawazito, hata wanakuwa hatarini, kwani kwa kiasi kikubwa ugonjwa huo unasababisha kutoka kwa mimba

Kwa mujibu wa Shirika la Chakula Duniani (FAO), magonjwa yatokanayo na wanyama yameongezeka kwa binadamu.

FAO inafafanua mlipuko wa magonjwa duniani umezidi kubadilika, kutokana na kuongezeka idadi ya watu, kupanuka kilimo na hata usambazaji wa chakula FAO

Ripoti ya shirika hilo hivi karibuni, inasema ni muhimu kuwapo mpango wa pamoja kudhibiti tishio la magonjwa yatokanayo na wanyama, kwani binadamu inawachukua kwa asilimia 70 ya magonjwa yanayoibuka hivi karibuni.

Katika nchi zinazoendelea, zinatajwa kuwa hatarini kutokana na mwingiliano wa magonjwa ya binadamu na wanyama, hata inatishia usalama wa chakula.

Mkurugenzi Msaidizi wa FAO, Ren Wang anafafanua umuhimu wa kushughulikia kwa pamoja afya ya binadamu na wanyama, pia mazingira katika kuchambua chanzo cha magonjwa.

Bila shaka tusiache kufuga wanyama hao ambao ni kama mapambo na sehemu ya faraja na wengine wao ni kiini cha kipato, isipokuwa ni muhimu kuzingatia kanuni za afya ili kuepuka magonjwa hatarishi yanayotokana wanyama.

## HABARI KITAIFA

# Vigogo 14 kizimbani mashtaka uhujumu bil. 2/-, yumo DED

**Na Neema Hussein,** KATAVI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Katavi, imewafikisha mahakamani watuhumiwa 14 akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi, Catherine Mashalla.

Watumishi hao wamepandishwa kizimbani kwa mashtaka ya uhujumu uchumi na kuisababishia halmashauri kupata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Walipandishwa jana kizimbani na kusomewa mashtaka 153 yakiwamo ya uhujumu uchumi, kuunda genge la uhalifu, utakatishaji wa fedha na kughushi kwa njia ya mtandao kwa kufanya malipo kinyume cha utaratibu.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rebecca Mwalusako katika Mahakama ya Wilaya ya Mpanda, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Kelvin Mwaja, alidai kuwa watu hao wameshtakiwa kwa uhujumu uchumi.

Mwaja alidai kuwa washtakiwa kwa nyakati tofauti, walihamisha fedha kutoka akaunti ya halmashauri kwenda kwenye akaunti za watu binafsi huku wakijua ni kinyume cha utaratibu.

Baada ya kusomewa mashtaka, Hakimu Mwalusako alisema mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo kutokana na aina ya kesi hiyo. Aliahirisha kesi hadi Machi 28 atakapotajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Katavi.

Hata hivyo, washtakiwa hao waliiomba mahakama kuharakisha kusikiliza shauri lao kwa kuwa tangu wakamatwe ni mwezi wa nane na halijaanza kusikilizwa hali ambayo inawafanya kupoteza muda wakiwa mahabusu.

# Leseni mbili uwekezaji wa Dola milioni 628 uchimbaji, uchenjuaji madini zatolewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



SERIKALI imekabidhi leseni mbili za uchimbaji madini na kiwanda cha uchenjuaji ambazo uwekezaji wake unakadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 627.7.

Katika mradi huo unaotarajiwa kuzalisha ajira na kuiongezea serikali mapato, leseni zimetolewa kwa kampuni za Nyati Mineral Sands Limited itakayochimba madini ya tembo katika eneo la Tajiri, Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga na leseni ya ujenzi wa kiwanda cha uchenjuaji madini ya metali mkoani Shinyanga kwa Kampuni ya Tembo Nickel Refining Company Limited.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, (pichani) alisema hayo jana jijini hapa kuwa katika kampuni hizo, serikali inamiliki hisa kwa asilimia 16 kwa kila kampuni.

Alisema Kampuni ya Nyati itawekeza Dola za Marekani milioni 127.7 na mradi utaanza kuzalisha faida baada ya miaka minne na miezi sita.

Alisema uwekezaji huo utakuwa na manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na serikali kukusanya mapato takribani Dola za Marekani milioni 437.96 kutokana na gawio la hisa za serikali, kodi na tozo mbalimbali.

Alisema uwekezaji huo utazalisha fursa za ajira za moja kwa moja 150, kuongeza fursa za biashara na kuimarisha hali ya uchumi na ustawi wa jamii kutokana na kuwapo miradi ya huduma za jamii zitakazotolewa kupitia utaratibu wa CSR.

"Uchenjuaji wa makinikia ya heavy mineral sands utazalisha madini kama zircon, leucoxene, rutile, garnet monazite na ilmenite. Heavy Mineral Sands hutumika kutengeneza mapambo, vifaa tiba, vifaa vya nyuklia, injini za ndege, saa, simu, kompyuta mpakato na vyungu vya kuyeyushia metali na soko kubwa la madini hayo kwa sasa ni katika nchi za Marekani, China, Japani, Korea, India na Afrika Kusini,"alisema.

Kuhusu leseni ya kiwanda cha usafishaji wa madini, Mavunde alisema takribani Dola za Marekani milioni 500 zitawekezwa katika kiwanda hicho kitakachotumia teknolojia ya hydrometallurgy ikiwa ni mbadala wa technolojia ya uyeyushaji (smelting) na hivyo kuwa na gharama nafuu za uendeshaji na uzalishaji bora wa metali baada ya uchakataji.

Alisema kuwa kupitia teknolojia hiyo, makinikia yatakayozalishwa kwa njia ya flotation katika mgodi wa Kabanga na mingine nchini, yatachakatwa na kuzalisha metali zenye ubora wa asilimia 99.9.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Batilda Buriani alisema mkoa una kiasi kikubwa cha rasilimali madini ya tembo, hivyo kupitia leseni hiyo utajiri utaongezeka na Pangani itafunguka kiuchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha alisema uwekezaji wa kiwanda hicho cha kuchenjua madini utasaidia kubadili sura ya Kahama kwa kuongeza fursa za ajira kwa wananchi.

Mtendaji Mkuu wa Life Zone Metals, Chris Showalter alisema lengo lao ni kuongeza thamani ya nikeli, shaba na kopa nchini ili mikono ya Watanzania ndio ijenge mustakabali wa nchi.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

### KUHUSU WAMILIKI WA VYOMBO VYA MOTO VYENYE USAJILI WA NAMBA BINAFSI ZA JINA

**Dares Salaam, 21 Machi, 2024:**
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuutaarifu umma kuwa usajili wa vyombo vya moto. yaani magari na pikipiki. kwa namba binafsi za jina (Personalised Number Plate) hudumu kwa kipindi cha miaka mitatu ambapo baada ya muda wa ukomo wa usajili husika. mmiliki wa chombo cha moto anapaswa kulipia tena ada ya kuhuisha usajili kwa kipindi kingine cha miaka mitatu au kutoa notisi kwa Kamishna ya kuomba kusitisha huduma hii. Utaratibu huu unatekelezwa kwa mujibu wa sheria ya Vyombo vya Moto ya Mwaka 1972.

Hata hivyo. Mamlaka imebaini uwepo wa wamiliki wa vyombo vya moto vilivyosajiliwa kwa namba binafsi ambao wanaendelea kutumia vyombo hivyo bila kulipia ada ya kuhuisha usajili husika.

Hivyo basi. TRA inatoa rai kwa wamiliki wote wa vyombo vya moto wenye malimbikizo ya madeni ya kodi yatokanayo na usajili wa namba binafsi za jina kufika katika ofisi za TRA zilizopo kila mkoa na kutekeleza yafuatayo;-

1. Kupata taarifa ya malimbikizo ya madeni (mchanganuo) tangu muda wa matumizi ya namba binafsi za jina ulipoisha hadi sasa.
2. Kufanya malipo ya malimbikizo ya madeni yatokanayo na utumiaji wa namba binafsi za jina ama kuwasilisha nyaraka zitakazothibitisha hadaiwi. mfano stakabadhi ya malipo.
3. Kutoa taarifa ya kusudio la kusitisha l kuhuisha matumizi ya namba binafsi za jina kabla ya muda wa miaka mitatu kwisha tangu mmiliki apate usajili wa namba binafsi za jina.
4. Mmiliki afike Ofisi ya TRA mnamo au kabla ya tarehe 31 Machi. 2024 akiwa na nyaraka zifuatazo;-

- Kadi halisi ya usajili wa Namba binafsi za jina.
- Nakala ya Kitambulisho cha mmiliki cha NIDA/Leseni ya udereva.
- Barua ya kusitisha /kuhuisha matumizi ya namba binafsi za jina.
- Kulipia gharama ya kurudisha usajili wa namba ya awali ama kuhuisha matumizi ya namba binafsi za jina.

Wamiliki wote wanataarifiwa kuwa kutafanyika zoezi la ukaguzi vyombo vya moto kwa ajili ya kubaini wale wote ambao wamelimbikiza madeni kwa magari yenye usajili wa namba binafsi za jina (Personalized Number Plate) pasipo kulipa kodi zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria.

Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na kituo cha huduma kwa walipakodi kwa kupiga simu za bure: **0800-780 078 / 0800-750 075 / 0800-110 016**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**
**Imetolewa na;**
**Idara ya Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano**
**TRA MAKAO MAKUU**

# Miaka Mitatu ya Rais Samia Madarakani ilivyoimarisha Sekta ya Benki nchini



Na Abdulmajid Nsekela,
**Mkurugenzi Mtendaji Benki ya CRDB**

Ule msemo wa kiingereza unaosema **'Give credit where its due'** waswahili wameupa tafsiri ya **'Mpeni maua yake,'** ukisisitiza utamaduni wetu wa kutambua mchango au jitihada za mtu angali bado yupo.

Ingawa msemo huu huenda usipate nafasi katika vyumba vya mikutano katika ngazi za juu, ninaona inafaa kuutumia sasa kama ishara ya shukrani kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake wa kipekee katika kipindi cha miaka mitatu ya utawala wake.

Wakati Rais Samia anaingia madarakani, tarehe 21 Machi 2021, Tanzania kama ilivyokuwa kwingineko duniani, ilikuwa inapambana na athari za janga la UVIKO-19 lililoukumba ulimwengu. Athari hizi ziliyagusa maeneo mengi ya uchumi, ikiwamo sekta ya benki. Sekta ya utalii na viwanda, biashara na wajasiriamali wadogo na wa kati wanaounda sehemu kubwa ya wateja wa benki na taasisi za fedha nchini, nao hawakubaki salama.

Wakati wachumi na wataalamu wa mipango wakitafuta namna ya kujiokoa katika hali hiyo, Rais Samia aliweka mikakati kadhaa ya kulivusha taifa lililokuwa linashuhudia mdororo kwenye sekta karibu zote hasa utalii na biashara ndogo na za kati ambazo sio tu ndizo zinaunda uchumi wa taifa letu bali zinaajiri Watanzania wengi zaidi. Tarehe 10 Oktoba 2021 alizindua Mpango wa Kufufua Uchumi dhidi ya Athari za UVIKO-19 ukitengewa Sh3.62 trilioni. Uzinduzi wa mpango huu ulienda sambamba na uboreshaji wa sera za fedha uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Matunda ya mpango huo yanajidhihirisha na sasa kila mmoja anajivunia hilo hasa sekta ya benki ambayo ilivuka salama na inaendelea kutoka mchango wake kwenye uchumi.

Ili kuharakisha kufufua uchumi ulioathirika na janga la UVIKO-19, serikali kupitia BoT ilianzisha mfuko maalumu ikitenga Sh1 trilioni kwa ajili ya kuzikopesha benki za biashara zinazotoa mikopo kwa wakulima. Hatua hii ilikusudia kuzifanya benki zitoe mikopo nafuu kwa wakulima ikipendekeza kutoza riba ya tarakimu moja. Benki ya CRDB ilitekeleza pendekezo hili kwa haraka ikawa ya kwanza kutangaza riba ya asilimia 9.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Viongozi mbalimbali pamoja na Wananchi wakati wa uzinduzi wa Filamu ya Tanzania The Royal Tour uliofanyika katika Ukumbi wa JNICC Jijini Dar es Salaam tarehe 08 Mei, 2022



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza akichangia jambo wakati wa majadiliano katika Mkutano Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) unaofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) tarehe 07 Septemba, 2023.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na Mkurugenzi Mkuu wa Proparco, Jean Chalard wakionyesha mikataba yenye thamani ya Sh 182 bilioni ya kuwawezesha wajasiriamali walioathirika na janga la UVIKO-19 nchini, 29 Mei 2022.

Ndani ya kipindi hiki cha miaka mitatu, thamani ya mikopo iliyotolewa na Benki ya CRDB kwenye sekta ya kilimo imeongezeka kutoka Sh647.229 bilioni mwaka 2021 mpaka Sh1.347 trilioni mwaka 2023. Hili sio tu limewanufaisha wakulima husika bali limesaidia kuboresha na kuimarisha miundombinu muhimu hivyo kuihakikishia Tanzania chakula cha kutosha.

Msimamo wa Rais Samia kuhusu diplomasia ya uchumi sio tu kwamba umewezesha taasisi kama Benki ya CRDB kujitanua katika nchi jirani kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) lakini pia umekuza ushirikiano katika sekta ya fedha, na kuvutia fedha za ziada ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kutokana na jitihada hizo, Benki ya CRDB imesaini mikataba yenye thamani ya zaidi ya Sh700 bilioni na mashirika tofauti ya kimataifa likiwamo Proparco, USAID, Mfuko wa Dhamana Afrika (AGF), Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), AFRIEXIM, na Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC). Mikataba hii yote imefanikishwa kutokana na imani waliyonayo wawekezaji wa kimataifa juu ya Tanzania.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na mgeni wake Makamu wa Rais wa Marekani Mhe. Kamala Harris wakati walipokuwa wakizungumza na Waandishi wa Habari wa Tanzania, Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 30 Machi, 2023.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan (watatu kushoto) akipata maelezo ya ujenzi wa soko la kisasa Kizimkazi Dimbani linalojengwa kwa ufadhili wa CRDB Bank Foundation katika hafla iliyofanyika Agosti 29, 2023, Zanzibar.



Naibu Gavana wa Benki Kuu DRC, Dieudonné Alimasi (watatu kushoto) akikabidhi leseni ya kutoa huduma za kibenki nchini humo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Jessica Nyachiro. Wakishuhudia zoezi hilo ni viongozi waandamizi wa Benki ya CRDB.

# Miaka Mitatu ya Rais Samia Madarakani ilivyoimarisha Sekta ya Benki nchini



Juhudi za uongozi wa Mheshimiwa Rais pia zimesababisha ongezeko kubwa la matumizi ya huduma za kibenki, huku Finscope 2023 ikiripoti kuongezeka kwa ujumuishi wa kibenki hadi asilimia 22 kutoka asilimia 17 iliyorekodiwa mwaka 2017.

Hii inathibitishwa na idadi ya mikopo iliyotolewa na sekta ya benki. Mikopo katika sekta mbalimbali za maendeleo nchini imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, thamnani ya mikopo iliyotolewa na Benki ya CRDB imeongezeka hadi kufikia Sh8.269 trilioni mwaka 2023 kutoka Sh5.148 trilioni mwaka 2021.

Katikati ya ukuaji huu, jumla ya mali za Benki ya CRDB imeongezeka kwa asilimia 88, kufikia Sh13.3 trilioni mwaka 2023. Ukuaji wa mikopo umeongezeka kwa asilimia 118, wakati mikopo chechefu ikiwa imezibitiwa ipasavyo ndani ya viwango vya udhibiti.

Wateja wanaporejesha mikopo yao kutokana na mazingira mazuri katika soko, ufanisi wa uendeshaji unaendelea kuimarika. Hii imepelekea, uwiano wa gharama kwa mapato, ambao ulikuwa asilimia 61.6 mwaka 2020, ulishuka hadi asilimia 49.5 mwaka 2023.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuashiria uzinduzi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha kutoka Mwanza hadi Isaka km 341.*




*Waziri wa Uwekezaji na Mipango, Prof Kitila Mkumbo (katikati), pamoja na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, na Wakurugenzi Wakuu wa CMSA na DSE wakati wa hafla ya uzinduzi 31 August 2023.*

Kwa upande mwengine, amana za Benki zimekuwa kwa asilimia 64 kufikia Sh8.86 trilioni mwaka 2023 kulinanisha na Sh5.4 trilioni mwaka 2020. Jambo jema ni kwamba, ukuaji si tu umewahahikishia wateja upatikanaji wa mikopo ili kuchochea biashara zao, bali pia utendaji bora ambao matokeo yake yanaonekana katika uwekezaji wa wanahisa.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, faida ya sekta ya benki imeonekana kuongezeka kwa kiwango kikubwa. Mwaka jana 2023 Benki ya CRDB ilirekodi Faida Baada ya Sh424 bilioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 58.2 kutoka Sh268 bilioni iliyorekodiwa mwaka 2021.

Ufanisi ulioshuhudiwa kwenye sekta ya fedha, umeziwezesha benki kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa miradi ya kimkakati mfano ujenzi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), pamoja na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambayo imesaidia kuipandisha hadhi ya Tanzania kimataifa hivyo kuvutia wawekezaji wengi kutoka nje.

Nidhahiri kuwa uongozi wa Rais Samia umekuwa na jukumu muhimu katika kuchochea mwelekeo huu wa ukuaji, kuweka njia ya kuleta mabadiliko na kuboresha maisha ya watu kote Tanzania.

Kujitolea kwa Rais katika uwezeshaji wa vijana na wanawake pia kumechochea uvumbuzi katika sekta ya kifedha. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, tumeshuhudia kuimarishwa kwa majukwaa ya uwezeshaji wanawake nchini kote. Programu ya Kilimo Biashara kwa Vijana (BBT) pia inaonyesha kujitolea huko kwa Rais katika kuwainua vijana kupitia kilimo.

Kwa kuzingatia maono ya rais, taasisi yetu ya CRDB Bank Foundation ilizindua programu ya iMbeju, ikitoa mafunzo, ushauri, mitaji wezeshi, na msaada unaohitajika ili kuinua biashara zinazomilikiwa na wanawake na vijana. Kufikia Januari 2024, taasisi hiyo ilikuwa imetoa mafunzo kwa zaidi ya vijana na wanawake 150,000 na kutoa jumla ya mitaji wezeshi yenye thamani ya Sh5 bilioni.

Eneo lingine ambalo limechochea uvumbuzi ni ufadhili wa miradi ya kijani na ile inayozingatia mabdiliko ya tabianchi. Tangu aingie madarakani, Rais Samia ameweka kipaombele katika utunzaji wa mazingira huku akipambana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Amekuwa akihudhuria kikamilifu mikutano ya mabadiliko ya hali ya hewa, ikiwa ni pamoja na mkutano wa COP28 uliofanyika Dubai mwaka jana, ambapo alizindua Mradi wa Nishati Safi ya kupikia itakayowasaidia Wanawake Barani Afrika (AWCCSP).

Tukiwa Benki kiongozi ya kizalendo, Benki ya CRDB inaongoza kwa kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuja na ubunifu wa bidhaa maalum kwa ajili ya ufadhili wa miradi ya kijani. Mwaka jana, benki yetu ilitoa hatifungani ya kwanza ya kijani nchini, 'Kijani Bond', ikiwa ni hatifungani kubwa zaidi katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Katika awamu ya kwanza ya mauzo yake, Hatifungani ya Kijani iliingiza Sh171.82 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 429.57 kutoka Sh40 bilioni zilizokusudiwa awali. Sio tu mafanikio haya yalivuka malengo bali yalidhihirisha imani waliyonayo wawekezaji wa ndani na wale wa kimatifa.

Rais Samia anadhihirisha hili kutokana na mikakati anayoiweka na kuitekeleza katika kuujenga uchumi wa Tanzania akiacha alama katika sekta tofauti za uchumi ikiwamo ya fedha. Tunampongeza na kumshukuru kwa juhudi hizi za kuliendeleza taifa letu.

**Mjasiriamali wa Marekani Anne Wojcicki aliwahi kusema,**

> "Njia pekee ya kiongozi kuleta mabadiliko ni pale unapoongoza kwa mfano. Ikiwa unataka kila mtu awe na shauku, kujitolea, na kuhamasishwa, unatakiwa kufanya kwanza."





# Kamati yamvutia kasi mkandarasi wa kusambaza umeme

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imesema haijaridhishwa na kasi ya ujenzi na usambazaji wa miundombinu ya umeme katika vijiji 146 wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Imesema hali hiyo inasababisha wananchi kukosa nishati hiyo na kushindwa kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani mazao vijijini.

Mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya Tontan Project Technology Co. Ltd Jv Group Six International kupitia mradi wa uwekezaji wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili.

Akizungumza na wananchi katika Kata ya Wendele Manispaa ya Kahama wakati kamati hiyo ilipofanya ziara ya kukagua thamani ya mradi, Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga alisema kasi ya mradi huo ipo chini sana.

Alisema kamati imebaini kati ya vijiji hivyo ni vijiji 63 pekee vilivyopatiwa umeme katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama.

Hasunga alisema serikali kupitia Bunge waliidhinisha Sh.bilioni 46.092 kwa ajili ya usambazaji wa umeme katika vijiji vya Wilaya ya Kahama na mradi uliotarajiwa kukamilika Aprili 30 mwaka huu.

Alisema lakini mpaka sasa kasi yake ni ndogo na imesalia mwezi mmoja tu, hivyo kamati haijaridhiwa na mkandarasi, akisema wanaoendelea kuumia ni wananchi.

"Wananchi wengi bado hawajapata umeme vijijini, Mei mwaka huu tutarudi tena kuangalia kama wameunganishiwa wote na ndipo tutakapotathmini na kupima kama fedha zilizotolewa ni sawa na thamani ya mradi huu,"alisema Hasunga.

Mkurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Jones Olotu akitoa taarifa ya utekelezaji na usambazaji umeme alisema, Shinyanga ina vijiji 509 kati ya hivyo 262 vimepatiwa huduma, huku Wilaya ya Kahama ikiwa na vijiji 146 kati yake vijiji 63 vinaumeme na vimebaki vijiji 83.

Mkaguzi Mkuu wa Nje kutoka Wizara ya Nishati, Nyamisi Bituro alisema ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imebaini kuwepo kasi ndogo ya ujenzi na usambazaji wa umeme licha ya kupewa muda wa nyongeza wa miezi minne mfululizo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama Mboni Mhita alisema kucheleweshwa kukamilika kwa mradi kunasababisha viongozi wa siasa, serikali kuchonganishwa na wananchi kutokana na ahadi za mara kwa mara juu ya upelekaji umeme kwa wananchi.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita akizungumza na wajasirimali wadogo wa kituo kidogo cha mabasi Kahama CDT jana, wakati wa hafla ya kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwawezesha kupata eneo la kufanya biashara zao na fedha za mikopo isiyokuwa na riba ili kuondokana na mikopo umiza. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Vijana 100,000 wafundwa kujikinga maambukizi VVU

**Na Timothy Itembe,** TARIME

VIJANA zaidi ya 100,000 kutoka mkoani Mara wameanza kupewa elimu rika kwa lengo la kuwasaidia kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), sambamba na kupata elimu ya afya ya uzazi.

Akizungumza wakati wa utolewaji wa elimu hiyo kwa vijana zaidi ya 40 kutoka wilayani Tarime, Ofisa Mradi kutoka shirika lisilo la kiserikali la Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF), Anold Masawe alisema hatua hiyo itasadia kupunguza ama kumaliza maambukizi mapya ya VVU ifikapo mwaka 2030.

Alisema lengo lao ni kuwafikia vijana zaidi ya 100,000 kwani kundi hilo ndilo lipo hatarini zaidi kuambukizwa na virusi hivyo, na kuwataka vijana waliopata mafunzo hayo kuhakikisha wanakuwa mabalozi kwa jamii zinazowazunguka ili kurahisisha kazi hiyo.

"Tunatarajia kufikia kundi la vijana laki moja hivyo kupitia hawa tuliowapatia elimu wataendelea kuwa mabalozi wazuri nasisitiza jamii kuendelea kuwapa ushirikiano ili kufikia malengo ya mradi na dhima ya serikali ifikapo mwaka 2030 kusiwepo na maambukizi mapya ya VVU," alisema Anold.

Baadhi ya vijana walioelimishwa akiwemo, Ghati Nyamohanga alisema elimu hiyo inatakiwa pia kupelekwa kwa wachungaji ambao wamekuwa wakiipotosha jamii kwa kujinadi kuwa wanaponya UKIMWI na kuwakataza wagonjwa kutumia dawa.

Kenedy Julius kutoka Nyamirbaro alisema elimu hiyo imekuja kwa wakati, hivyo jukumu lao kama vijana ni kuhakikisha wanaifikisha katika jamii ili kuisaidia kujikinga dhidi ya VVU.

# RC mpya aanza na utatuzi wa migogoro ya ardhi, atoa maagizo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Annamringi Macha, amewaagiza maofisa ardhi kutoka halmashauri za mkoani hapa kutoka ofisini na kuwafuata wananchi na kutatua kero za migogoro ya ardhi pamoja na kuzitatua.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa hafla ya kukabidhiwa ofisi na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, ambaye ameteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Alisema katika maagizo waliyoyapokea kutoka kwa Rais Samia wakati akiwaapisha ni pamoja na kusikiliza na kutatua kero za wananchi hasa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa mingi, hivyo kuwataka maofisa hao kujipanga katika uwajibikaji huo.

Pia aliwasisitiza viongozi kila mmoja afanye kazi kwa bidii katika eneo lake na kuwatendea haki wananchi, pamoja na kuwapatia elimu ya kufanya kazi kwa bidii na kujipatia kipato hasa vijana, na siyo kushinda wakicheza kamali pamoja na wazee kucheza bao.

Aidha, aliwataka pia watendaji wa serikali wasijihusishe na masuala ya siasa na kuanza kutafuta nani wa kuwaongoza hasa kwenye kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani, kwamba jambo hilo waviachie vyama vya siasa, huku akiwasihi kufanya kazi bila mafarakano na chuki.


Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Christina Mndeme, ambaye kwa sasa ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, aliwashukuru watumishi wa Serikali mkoani hapa kwa kumpatia ushirikiano, huku akiwasihi pia wampatie ushirikiano (Macha) ili kusukuma maendeleo ya Shinyanga.

Aidha, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Shinyanga hasa wanawake, kujikita zaidi katika kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na kutunza mazingira kwa kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassani katika utunzaji wa mazingira.




Ukurasa 12

Wasiowahi kuwa na barabara lami, wakenua meno mradi kuanza rasmi



Ukurasa 13

Wachambuzi wa michezo simile na Kiswahili chetu!



Ukurasa 14

**Vigezo 6 kumfanya mtu ajiamini kazini**


# BUFE

IJUMAA MACHI 22, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA

# Mtaji reli kisasa TRC, ubia wake na sekta binafsi, nchi kuwa kitovu uchumi

**Na Pilly Kigome**

• Soko linalolengwa; EAC, COMESA na SADC




Treni ya kisasa ilipofanyiwa majaribio mwezi uliopita. **PICHA: MAKTABA**

HIVI sasa inapojadiliwa mada, jicho la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan liliko katika kufikia maendeleo ya kisasa leo hii, hapana shaka ni katika orodha ya ubunifu, mwendelezo na maboresho ya miundombinu ya reli nchini.

Katika hilo kuna maeneo makuu mawili, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), ambayo reli yake inaanzia Dar es Salaaam, ikigota hadi bandarini na nchini Zambia mjini Kapirimposhi,

Pia, kuna reli chini ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), ambayo nayo inaanzia bandarini, inagawanyika katika njia nne, mosi Kaskazini, inayofika hadi bandarini Tanga na nyingine Arusha; Pia,'reli ya kati' zinazogota bandari za Kigoma, pia Mwanza.

Reli hiyo ya Kati, ndio Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anapambana nayo kuliongoza taifa, katika mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), ukiwa na gharama kubwa, pia ukitarajiwa kutoa matunda makubwa.

Katika kutekeleza Sera ya Viwanda na kuifikisha nchi kwenye Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025, harakati zilianza kwa serikali ikifanya marekebisho ya Sheria Reli ya Mwaka 2017, kuweka mpango mkakati wa kushirikisha sekta binafsi kwenye uendeshaji wake na utoaji huduma za usafirishaji kupitia miundombinu ya reli.

Mwenendo kuelekea miaka saba baadaye, Tanzania inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, inaendelea na ujenzi wa reli yenye kiwango cha kimataifa - SGR.

Matarajio yaliyoko ni ujenzi utakapokamilika, mtandao wake wa kilomita 2,102, utaunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Simiyu, Shinyanga, Mwanza na Kigoma.

Lengo ni kuziunganisha nchi zisizokuwa na bandari Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

### BOSI WA TRC

Akifafanua kuhusiana na miradi mikubwa ya TRC, Mkurugenzi Mtendaji, Masanja Kadogosa, anasema ujenzi wa reli SGR unaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza Afrika kujenga mtandao mrefu zaidi wa reli barani Afrika.

Anasema, Tanzania inaingia kwenye historia ya kujenga reli itakayotumia nishati umeme na yenye mwendo kasi wa kilomita 160 kwa sasa, treni za abiria na kilomita 120 kwa treni za mizigo.

Mkurugenzi huyo anasema lengo la kushirikisha sekta binafsi, ni kuiwezesha serikali kuhudumia shehena nyingi, ikiwamo kuongeza ufanisi na ushindani utakaomwezesha mwananchi kupata huduma ya uhakika na bora zaidi.

Hadi sasa, serikali imeshawekeza katika ujenzi wa bandari kavu na vituo vya treni za mizigo katika maeneo yenye bandari kavu, lengo ni kuwavutia wafanyabiashara kutumia usafiri wa reli.

Anafafanua, pia kuwapo ujenzi wa vituo vikubwa vya kupangia treni za mizigo vilivyopo (Marshalling Yard), iliyopo eneo la Ihumwa jijini Dodoma.

Kadogosa anataja kwamba unasaidia kwa kiasi kikubwa usafirishaji mizigo kwenda nchi jirani za Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC), Rwanda na Burundi.

Pia, anataja kuwapo bandari kavu katika maeneo anayoyataja: Kwala mkoani Pwani; Ihumwa - Dodoma; Isaka- Shinyanga; Fela mkoani Mwanza na Katosho mkoani Kigoma

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Kadogosa, ushirikiano unaoendelea una dira kuifanya TRC ijiendeshe kwa mapato kutoka sekta binafsi na kujiotosheleza kwa njia za reli, injini za treni na mabehewa, hata usafirishaji wake kuwa wa haraka, salama na wenye ufanisi.

Pia, ni namna serikali inatarajiwa itajipatia faida kwa kupitisha mizigo ya nchi jirani, hata kujipatia fedha za kigeni.

### RELI YA KISASA

Mkurugenzi anataja ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa, unachangia Tanzania ikaendeleza ushirikiano mzuri na sekta binafsi, katika kuongeza pato lake la taifa.

Eneo lingine analolitaja, ni ushirikishwaji sekta binafsi kwenye uwekezaji na uendeshaji miundombinu ya reli, utaweka imani ya mfanyabiashara kuwa na uhakika wa kusafirisha mizigo bila shaka ya upungufu wa mabehewa.

Mpango huo unaoangukia mikakati ya Rais Dk. Samia, ni kwamba, utaongeza ufanisi katika matumizi ya miundombinu ya reli na huduma za usafirishaji relini, ikiondolewa fikra ya kuwapa ushindani kati ya serikali na sekta binafsi.

### TRC KATIKA PPP

Mkakati huu katika hilo, taarifa ya TRC inafafanua ni kuunganisha sekta ya umma na binafsi, kuongeza ufanisi wa usafirishaji na kuleta chachu ya maendeleo ya biashara nchini.

INAENDELEA UK.14

BIASHARA/UCHUMI

# Tuzo TWCC zinavyowafanya kinamama kuupiga mwingi biashara hadi ughaibuni

**Na Joseph Mwendapole**

TUZO zinazotolewa na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), zimefikisha mwaka wa nne zikiwa na mafanikio lukuki tangu kuanzishwa miaka minne iliyopita.

Sasa ni chachu kwa wanawake wafanyabiashara ya uzalishaji bidhaa na kuongeza mitaji, kurasimisha biashara, wengine wakianzisha kampuni.

Pia, TWCC imedumu kiungo muhimu kwa wanawake wafanyabiashara, ikiwapa taarifa za masoko, bidhaa za kuzalisha na namna ya kuzingatia viwango kitaifa na kimataifa.

Mwajuma Hamza, Mkurugenzi wa TWCC, anasema wanawake wafanyabiashara nchini wanaendelea kukua kila siku, hata vinara wa biashara mbalimbali.

Anaeleza, TWCC inawawezesha kinamama kuyafikia masoko nchini, Afrika Mashariki, bara Afrika, Ulaya na Marekani.

Mwajuma anataja kuwapa mbinu kumewapa ujasiri wanawake kufanya mambo makubwa, wakichuana na wanaume na hawaikatie tamaa kwa biashara zao.

Zao lake anataja kinamama wanaanzisha kampuni zenye ufanisi sokoni, wiki iliyopita badaji yao walitunukiwa tuzo za umahiri.

Anataja kampuni nyingi za wanawake zilizopewa tuzo ni za nishati, gesi, utoaji huduma, biashara na uzalishaji bidhaa za viwandani.



Kinamama wajasiriamali wakiwa kazini. **PICHA MTANDAO**

### WAZIRI PROF. MKUMBO

Mgeni rasmi kwenye utoaji wa tuzo hizo, kwenye hafla jijini Dar es salaam, ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Profesa Kitila Mkumbo, anayesema wanawake wana uwezo mkubwa wa kutunza fedha, kulinganisha na wanaume na biashara zao nyingi zimeimarikaa.

Anasema, tafiti zinaonyesha biashara za wanawake zinaendelea kwa sababu ya kutafiti kabla ya kuanzisha, tofauti na wanaume wengi hawatafiti, hivyo hawafiki mbali. Profesa Mkumbo anasema, hata kwenye urejeshaji mikopo, imeshuhudiwa wanawake wana nidhamu, hivyo wanakopesheka kulinganisha wanaume,.

Anasema mwelekeo wa Sera za Uchumi kwa serikali sasa ni kuwa na uchumi unaokuwa kwa kasi, kumpunguzia mwananchi umaskini na kuleta ustawi na maisha bora kwa wote.

Profesa Mkumbo, anasema kuna tafiti zingine zinawasifu kinamama katika utunzaji fedha, kushinda wanaume; huku nako uuzaji bidhaa katika soko kimataifa, tafiti ziwataja kuwa juu kuwazidi kinababa.

"Hata wanaoongoza kuchukua biashara Guangzhou China ni wanawake, kwa hiyo mnaweza kuona namna wanawake walivyo na nguvu na hakuna sababu ya nyinyi kuwa wanyonge... kwa hiyo simameni na msonge mbele kwasababu mnaweza," anasema

Anataja changamoto nyingi za wanawake ni za kijamii na siyo kibaolojia, kwa sababu baadhi ya watu hasa wanaume wamekuwa wakiwakatisha tamaa wanawake wanapothubutu kufanya makubwa.

Anasema asilimia 90 ya wanawake wanaofanyabiashara kwenye nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania, wanafanya bila kurasimishwa, hivyo programu kama za TWCC zitawasaidia wengi kurasimisha biashara zao na kuingia kwenye mfumo rasmi.

### MWENYEKITI TWCC

Mercy Sila, anasema Chemba hiyo, ina matawi kitaifa hadi Zanzibar, ikiwa namna ya kuwarahisishia wanawake kupata huduma kila wanapokwama.

Anasema zamani, wengi walilalamikia uhaba wa masoko, lakini mazingira ya sasa, masoko ya bidhaa za Tanzania ni mengi.

Hukua akishukuru hatua za kiserikali, anafafanua: "Sisi wafanyabiashara wanawake sasa tunajiamini na tuna uthubutu wa kufanya mambo makubwa na Profesa wengi unaowaona hapa ni wakurugenzi kwenye kampuni zao walizoanzisha wenyewe."

Anasema, TWCC imekuwa ikiwapa taarifa wanachama wake kuhusu masoko na bidhaa zinazohitajika na wengi wameshaingia kwenye masoko ya Afrika Mashariki na kwingineko Afrika.

Anasema wanawake wengi wamekuwa kibiashara wakiwa na mitaji mikubwa, wanachoogopa kurasimisha bishara zao ni usumbufu kiserikali wa leseni na kodi.

Mwenyekiti huyo anasema TWCC inaendelea kuwaelimisha umuhimu wa kusajili biashara zao, wengi wanaonekana kuelewa somo hilo.

Pia, anahitimisha kuwa TWCC imefungua tawi kwa vijana wa kike na kiume wenye miaka chini ya 18 wakifundishwa ujasiriamali, hata watakapomaliza masomo wajiajiri, badala ya kuhangaika ajira.

### DIPLOMASIA UCHUMI

Mkurugenzi wa Biashara ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi katika Wizara ya Mambo ya Nje, John Ulanga, anasema TWCC, kuanzisha mpango uitwao 'Export Guarantee Scheme' kwa wanachama wake, iwe rahisi kwao kukuza biashara na mitaji.

Akitoa mada kuhusu 'Nafasi ya Mwanamke katika Maendeleo Endelevu, Balozi Ulanga, akasema hakuna mafanikio kijamii yanaweza kupatikana, iwapo kundi la wanawake wataachwa nyuma.

Mtaalamu huyo anasema, 'mpango wa dhamana kwa wanawake wafanyabiashara' ni muhimu, kwani wengi wanapata masoko ya bidhaa zao, lakini wanashindwa kukosa mtaji wa uhakika, hivyo mpango huo utakuwa mkombozi.

"Kuna mwenzenu mmoja hapa amepata zabuni ya kupeleka mkonge Ghana, lakini amekosa mtaji kama wa shilingi milioni 200. Sasa mngekuwa na mpango wa dhamana, mngemkwamua akapeleka bidhaa zake bila kikwazo," alisema

Ulanga anasema TWCC inaanzisha mpango huo kwa kushirikiana na mifuko ya serikali na taasisi binafsi za fedha, hata ukawa msaada kwa wanawake kukuza biashara zao.

"Najua nyuma huko tuliwahi kuwa na kitu kama hiki tukakwama," anasema Ulanga

Aidha, anaishauri TWCC kuandaa ripoti ya kila mwaka inayoelezea maendeleo ya wafanyabiashara wanawake na changamoto zao kwenye biashara, ikisaidia kufahamisha hatua zao na kusaidia mikakati imayowawezesha kusonga zaidi, huku ikihamaisha wanachama zaidi.

Vile vile, anawataka wanawake wafanyabiashara kuangalia fursa za masoko mengine ya Afrika, Ulaya na Marekani, badala kujikit6a nchini pekee.

"TWCC wasaidieni wanawake hawa kuratibu namna ya kuuza nje biashara zao (export strategy) na mzitumie balozi zetu mnapokwama," anawaasa, wasiogope.

### KUTOKA TANTRADE

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (Tantrade), Latifa Mohamed anaipongeza TWCC, akiwahakikishia wanawake hao fursa za masoko ya bidhaa zao.

"Mara nyingi utasikia wafanyabiashara wanalalamikia uhaba wa masoko, lakini niwahakikishie masoko yapo ni sisi kuyatafuta na ili kuyafikia, lazima tuwe wabunifu na tusiige vinavyofanywa na wengine...," anasema

# Wasiowahi kuwa na barabara lami, wakenua meno mradi kuanza rasmi

**Na Beatrice Moses**

NI TUKIO lenye majibu ya kilio cha kero za wakazi wa Kimara, Bonyokwa na Kinyerezi, Dar es Salaam, ambao hawajawahi kuwa na barabara ya lami.

Wamedumu na adha inayohatarisha afya zao kwa vumbi, wakati wa mvua wanatembea umbali mrefu, kwa kuwa magari na vyombo vingine vya usafiri haviwezi kufika hapo kutokana na utelezi wa tope.

Tarehe 9 mwezi huu, sasa wanaibatiza jina 'Furaha 'Day', kwani ndio kumefanyika makabidhiano ya nyaraka za ujenzi kutoka Wakala wa Ujenzi wa Barabara Tanzania (TANROAD) na Mkandarasi mjenzi, kampuni ya Nyanza Road Works.

Akisoma risala ya wakazi wenzake, Robert Salia, anasema kwa muda mrefu barabara hiyo imedumu changamoto, mvua zinaponyesha zaidi, wengi wanakosa uhakika kwenda kwenye shughuli zao za kujitafutia riziki.

"Ubovu wa barabara hii umeifanya Kata ya Kimara na maeneo jirani kuwa nyuma kimaendeleo, licha ya kuwa karibu na barabara kubwa ya Morogoro, Tabata, jirani na eneo la Ubungo ambalo lila fursa mbalimbali," anasema Salia

Anafafanua namna barabara imewatesa muda mrefu, hata wanahamia furaha kutengewa fedha za mradi tajwa, wakimwagiwa sifa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Salia anafafanua: "Tumeitwa majina ya utani mengi sana kutokana na kufika kazini tukiwa tumejaa mavumbi. Mradi huu unapoanza, tunaahidi kutoa ushirikiano katika hatua zote, kufanikisha ndoto hii."

Ombi walilo nalo sasa barabara hiyo iitwe Samia Highway, kuthamini uwezeshaji barabara tajwa, ambayo hadi sasa kando yake kuna biashara nyingi ndogo na hakuna uwekezaji mkubwa

"Katika Bunge la bajeti la mwaka 2022 sauti juu ya ubovu wa barabara hii zilipazwa zaidi na mbunge wetu Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Bona Mbunge wa jimbo la Segerea.

"Juhudi za wabunge wetu hawa katika nyakati tofauti, ziliibua majibu mbalimbali toka kwa mawaziri husika likiawemo la ahadi ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kadri serikali itakavyopata fedha," anasema.

Anasifu hatua mara ya kwanza barabara hiyo kuingizwa katika bajeti kuu serikalini, mwaka wa fedha 2023/2024, akitaja ni juhudi za wanachi na wabunge kufanikisha barabara kutangaziwa zabuni ya ujenzi Januari mwaka jana.

"Hadi tunafika hatua hii, tuna kila sababu ya kuamini kuwa barabara hii inaenda kujengwa kwa kiwango cha lami, katika Awamu ya Sita (ya Samia) tunashuhudia kutimia kwa ndoto ambayo hatukuitarajiwa na tulishakata tamaa.," anasema

Akifafanua ni mradi wenye urefu kilometa 14 kutoka mahali waliko kuelekea Kinyerezi.

Katika makabidhiano hayo, mgeni rasmi Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam Albert Chalamila akatoa anagalio dhidi ya watakaoweka kikwazo cha ujenzi, akisema:

" Nimeambiwa tayari kuna watu wamepangwa kwenda mahakamani kuweka zuio la ujenzi wa barabara hii, msihofu wananchi ole wao mahakama ione kuwa hawana haki!" anatamka Chalamila na kuendelea:

"Dakika tano nyingi, baada ya uamuzi kutolewa nitaweka greda zishushe nyumba zao, hatupendi watu wasiopenda maendeleo, wanaotumika kutukwamisha,".

Mkurugenzi wa Miradi wa Wakala wa Ujenzi wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Japherson Nnko, anaueleza mradi huo unaoendeshwa na mjenzi mzawa, una husisha kilomita sita za lami, ikiwekewa taa barabarani na itakamilika Julai, 2025.

Mbunge wa jimbo hilo Ubungo, Profesa Mkumbo, ambaye pia ni Waziri wa Uwekezaji, anasema shida ya barabara hiyo ilikuwa adha kubwa kwa wakazi wake, sasa anawarejesha imani ya uhakika wa safari zao kila wakati.


Mbunge wa jimbo Jirani la Segerea mbako Barabara inaishia, Bona Kamoli, anamtaka mkandarasi kutoa kipaumbele cha ajira zitakazojitokeza awape vijana wa maeneo hayo.




Tukio la kuidhinishwa mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo. **PICHA: BEATRICE MOSES**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wachambuzi wa michezo simile na Kiswahili chetu!





**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

TANZANIA katika historia yake, ilitawaliwa na Wajerumani, pia Waingereza, ambao ndio watawala wa mwisho wakawa ni Waingereza walioondoka nchini mwaka 1961 wakati pakiitwa Tanganyika.

Walituachia athari au kasumba fulani ya kimawasiliano na kitabia, ambazo baadhi yetu tulitaka kujifananisha nao Waingereza, kutenda na kuzungumza kama wao.

Tukathamini sana Kiingereza kuliko hata lugha za makabila yetu na hata kilipokuja Kiswahili kama lugha yetu ya Taifa, bado watu walijiona washamba kukizungumza.

Pamoja na kupigia debe lugha ya Kiswahili, pia za kikabila, bado baadhi yetu hatujioni kufika mpaka tuzungumze Kiingereza au hata majina kupeana ya Kiingereza au kigeni.

Leo tuna baadhi ya wasanii hata majina yao ya kuzaliwa tumeyasahau, sina haja hata ya kuwataja hapa, kwani wanajijua. Sijui nani aliwaambia bila kujipachika majina ya kigeni usanii wao si mali kitu?

Hivi sasa vitoto vinavyozaliwa katika hospitali zetu hizi, huwezi kukuta majina ya kienyeji, utadhani kadi za kliniki haziandikiki kwa majina hayo, lazima yawe kenye lafudhi za kigeni.

Kimichezo tunapiga hatua sana, hususan katika soka, masumbwi na kidogokidogo, riadha ambayo zamani tulikuwa mbele kuliko michezo mingine, lakini leo tunajongeajongea kidogo.

Maendeleo ya michezo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa pia na vyombo vya habari, hususan vya kilektroniki kama vile redio na luninga, ambako wengi hufuatilia michezo au matangazo mbashara.

Tunasikia karibu katika kila kituo cha luninga au redio, kuna uchambuzi wa michezo, ambao kila kituo kina wachambuzi wake ambao hufanya watazamaji na wasikilizaji kufuatilia nini kinaendelea nchini na duniani.

Vituo vingi kama si vyote, njia yao ya mawasiliano ni kwa lugha ya Kiswahili vikilenga kuwasiliana si tu na waishio mijini bali hata vijijini na si wasomi tu bali hata wasiosoma, lakini kikubwa ni Waswahili walioko nchini.

Nasema hivyo, kwa sababu si wengi waishio nje ya Tanzania wanaoweza kufuatilia vipindi vya Kiswahili isipokuwa kama ni Watanzania waishio nje ya nchi kwa majukumu au sababu maalumu.

Hapana ubishi kwamba, wachambuzi hawa wameisaidia sana jamii kitaarifa za michezo na sasa wengi wanajua nini kinafanyika wapi na lini na wakati gani na kuwa na shauku ya kufuatilia.

Tatizo lililopo ni mawasiliano baina ya wachambuzi wao kwa wao, pia na wasikilizaji wao, kwani kumekuwa na ugonjwa ule ule wa kusahau au kuharibu Kiswahili kwa kukichanganya na Kiingereza, ambacho wakati mwingine si sahihi.

Licha ya kukimbilia kuonesha kuwa wachambuzi wetu hawa ingawa si wote wanakijua Kiingereza, lakini hata hicho Kiswahili chenyewe kwao ni shida, mpaka mtu anajiuliza wamesomea au wamechukuliwa tu kwa kuwa wanajua michezo?

Katika kuchanganyachanganya lugha hizi, wamekuwa wakiwanyima wasiojua Kiingereza fursa ya kujua wanajadili na kuchambua nini katika vipindi vyao.

Tatizo ni kudhani kuwa kama hujatamka neno la Kiingereza kumaanisha jambo fulani, basi hilo jambo ama hulijui au hulimudu na hivyo ni aibu kwako mtamkaji, bila ya kufahamu kumbe ufanyavyo ndivyo unaharibu.

Inashangaza kusikia mathalan, mtangazaji anatamka straika (stricker), badala ya mshambuliaji. Utasikia sentabaki (center back) badala ya mlinzi wa kati. Utasikia spesi (space) badala ya nafasi, anakontroo (control) badala ya anadhibiti, na mambo mengi tu ambayo nafasi hii haitoshi kuyabainisha.

Lakini humo humo, utakuta sasa wanaobananga, mmoja nilipata kumsikia akitamka 'Conference Cup' akimaanisha Kombe la Shirikisho yaani 'Confederation Cup'! Huyu angetamka tu kwa Kiswahili moja kwa moja asingesumbua watu.

Mwingine alimkabili mwalimu wa kigeni asiyejua Kiswahili kumhoji kuhusu mchezo uliokuwa umemalizika punde na kuanza kumsalimia: "Kocha how are you?" Alitaka kusema Coach, lakini yeye akaibebesha Kiswahili.

Ni sawa, tunaweza kuwa tunataka kuonesha tunamudu lugha, lakini kumbe tunabananga vibaya mno. Ndiyo sababu hata ukifuatilia vipindi vingi vya michezo vina majina ya Kiingereza, utashangaa sababu ni nini?

Mbaya zaidi utasikia mtangazaji anasema 'kiwanda cha michezo'. Huyo anakuwa anatafsiri sisi kutoka maneno ya Kiingereza ya 'sports industry' badala ya tu kusema 'tasnia ya michezo'!

Sijagusa majina ya wachezaji kama Joseph Guede ambaye watangazaji wetu wengi wanamtamka Gwede badala ya Gede. Giroud ambaye wanamtamka Girudi badala ya Djiruu au Pacome wanayemtamka Pakome badala ya Pakom.

Inshalaah tutaelimishana na tutajua tu. Allah tusaidie. **Ramadhan Kareem!**

UCHUMI

# Vigezo 6 kumfanya mtu ajiamini kazini

**Na Mwandishi Wetu**



Watu wakiwajibika kazini. **PICHA: MTANDAO**

KAZI ni sehemu muhimu katika kushikilia na kutafsiri maisha ya mtu. Ndani ya tafsiri hiyo, ndiyo mtu huelekeza imani yake na baadhi hata kukosa kujiamini katika hofu 'ikipotea itakuwaje.'

"Sijui kwa nini bado hawajanifukuza. Wataona sifai kwa kazi hii. Niko hapa kwa bahati nzuri....," ni aina ya fikra huwafikia wafanyakazi wengi.

"Hali ya kutojiamini ni ugumu wa baadhi ya watu katika kutambua sifa zao wenyewe na mtazamo au hofu kwamba wengine wanaweza kugundua au kufikiri kuwa ni ulaghai.

"Inahusiana na hofu ya kutoishi kulingana na matarajio ya wengine," Dolors Liria, mtaalamu wa magonjwa ya akili na Makamu Mkuu wa Chama Rasmi cha Saikolojia ya Catalonia, Uhispania

Walikuwa wanasaikolojia Pauline Rose Clance na Suzanne Imes waliotoa hoja hiyo mara ya kwanza mwaka wa 1978, wakifafanua kwamba haishii akili pekee, bali hata uelewa unaotokana na kujifunza kihistoria.

Wanasaikolojia hao wanapendekeza, vigerzi muhimu katika kujiamini kazini;

1. Tambua tatizo; moja ya shida kuu ni kwamba hatuchukui wakati wa kuwasiliana na sisi wenyewe, kuungana na kile kinachotokea kwetu na kuchukua muda wa kufikiria juu yake.

Tunachojiambia na jinsi tunavyosema ni muhimu: "Lazima utambue kuwa haujithamini, haujui kusema 'nimefanya vizuri' au kujipongeza na haufikirii kuwa unastahili mafanikio haya," anasema Aranda. Ricart anasisitiza kwamba sauti hii ambayo inatuambia "hatutoshi", ilionekana wakati fulani katika maisha yetu "kama sauti ambayo ilitusaidia kuishi katika mazingira yetu". Huenda hata imetusaidia kufanya maendeleo katika mambo fulani, lakini tunapaswa kuwa waangalifu inapotuzuia kusonga mbele.

"Kujaribu kutafuta chanzo cha hili kunaweza kutusaidia kukabiliana na tatizo na kuona kama inavuka mipaka," anasema Dolors Liria.

2. Jikumbushe mafanikio yako; Mtazamo mdogo unaweza kusaidia tunapokuwa katika wakati wa dhiki kuu au kuzidiwa. Inaweza kusaidia kupunguza hisia hizi na kujitathmini kutokana na maoni ya kujenga zaidi.

Dolors Liria anapendekeza kukagua yaliyotupata katika matukio mengine wakati changamoto kama hizo zilipotokea. Unaweza kurejea akilini ukiwa na "mawazo haya ya kutojiamini" au unaweza hata kutengeneza orodha iliyoandikwa kwa mkono au kidijitali ya mafanikio yako yote.

"Ni aina ya kumbukumbu ya maendeleo ya kibinafsi, yenye mambo ya kufanya na wewe mwenyewe," anasema Aranda.

Mar Ricart anauita "mti wa mafanikio" na anaeleza kuwa ni muhimu ili tunaposahau mambo ambayo tumefanya, tunaweza kuungana tena na sehemu hiyo yetu sisi wenyewe.

3. Sherehekea kila mafanikio; Mara tu unapotimiza jambo fulani, unaendelea na jambo linalofuata bila kujipa nafasi ya kusherehekea, kuthamini, kujishukuru wewe mwenyewe kwa juhudi ulizoweka katika jambo hilo.

Ndiyo maana ni muhimu kusherehekea, kuishi na kutafakari mafanikio, haijalishi ni makubwa au madogo, kulingana na mtaalamu.

"Kwa sababu nyuma yake kuna gharama unayolipa, yaani juhudi. Na lazima ujipe nafasi ya kuiona, kushukuru kwa hilo na, kwa kweli kufurahia. Ikiwa sivyo, ni kana kwamba haipo."

Katika hali hii, "ni kuhusu kuunganishwa na mafanikio, na kuridhika, na kujisifu na kusema, 'Nilifanikiwa, nina furaha sana, ninastahili baada ya kupitia mengi'".

4. Jinsi watu wengine wanavyokuona; Mojawapo ya mambo yanayoashiria hali hii ni pengo kati ya kile unachofikiria juu yako mwenyewe na kile ambacho wengine wanafikiria kukuhusu.

Ndio maana inaweza kusaidia "kujiona kupitia macho ya wengine, kupitia kioo cha wengine," Aranda anasema. Mbali na kuwauliza watu wengine maswali, Aranda anapendekeza kuweka orodha ya yale ambayo wengine wanasema kukuhusu. "Andika unaposifiwa usisahau watu wanasemaje kuhusu kazi yako."

Zaidi ya hayo, ikiwa kuna shaka yoyote mahali pa kazi kuhusu jinsi tunavyofanya kazi, Dolors Liria ina pendekezo rahisi sana: uliza maoni.

"Tusisubiri watu watueleze tunaendeleaje, ukiwa na mashaka badala ya kusubiri waombe mameneja wakupe maoni kama huna uhakika unaifanya kazi hiyo vizuri au ukihitaji mtu wa kukuthibitishia."

5. Rekebisha matarajio; Katika uhusiano wowote kuna matarajio ya pande zote mbili. Bila shaka, hii inajumuisha mahusiano ya ajira: pande zote mbili zinatarajia kitu.

Lakini linapokuja suala la ugonjwa wa kutojiamini, matarajio yako yanaweza yasiwe yale unayotarajia kutoka kwa kazi yako, lakini yale unayotarajia kutoka kwako mwenyewe.

Anashauri kwamba tufanye zoezi ili kuona kama tunaweka matarajio ya juu sana, yasiyo ya kweli ambayo itakuwa ya kawaida kuhisi hofu ya kutoyafikia. Wacha tuchukue mfano rahisi: huwezi kutarajia kukimbia mbio za marathon katika miezi minne baada ya kuanza mazoezi.

Na katika hali hii, ni wajibu wa mtu aliye juu yetu kutupa miongozo wazi juu ya kile kinachotarajiwa katika kazi au kazi fulani "ili matarajio haya yaweze kurekebishwa".

6. Kujijali na kujihurumia; Kuhusishwa na hili ni kwa jinsi tunavyohisi, na jinsi tunavyotafakari na kujisikiliza - ni hali ya kujijali, ambayo wataalamu wanasema ni muhimu kwetu kufahamu kile kinachotokea kwetu na kujifunza jinsi ya kujidhibiti.

Michezo inaweza kusaidia na hii. "Ni muhimu sana kujidhibiti kihisia. Lakini si lazima uende kwenye mazoezi, inaweza kuwa kitu chochote kinachohusisha kusonga: kutembea au kucheza," anasema Liria. Tunapaswa kukumbuka umuhimu wa kuacha kazi na kuungana na mambo mengine, kama vile familia na marafiki. "Kuwa na njia ya kuungana ana kwa ana kunaboresha kujistahi kwetu."

"Ni muhimu kukuza jicho hili la huruma, kujiangalia wenyewe kwa upendo, kufanya marekebisho ya utambuzi wa mawazo ya kukosoa ambayo hali yako ya kutojiamini inakuambia."

• ***Kwa mujibu wa BBC***

## Mtaji reli kisasa TRC, ubia wake na sekta binafsi, nchi kuwa kitovu uchumi

**INATOKA UK.11**

**TRC KATIKA PPP**

Mkakati huu katika hilo, taarifa ya TRC inafafanua ni kuunganisha sekta ya umma na binafsi, kuongeza ufanisi wa usafirishaji na kuleta chachu ya maendeleo ya biashara nchini.

Wakati Rais Dk. Samia, akihimiza ubia na sekta hiyo, tayari serikali ina sheria, pia kuna sheriua na sera inayoongoza ubia kati ya sekta binafsi na umma, maarufu PPP huku ikianza kuwekezwa kwa wabia wa TRC, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Pia, siku chache zilizopita kuna uwekezaji wa vyombo vya usafiri katika Mamlaka ya Usafirishaji wa Reli wa Tanzania na Zambia (TAZARA).

Hadi sasa, inatajwa kumeanza kupokewa utashi wa baadhi ya kampuni za ndani na nje, zikivutiwa kuwekeza katika uendeshaji na utoaji huduma ya usafirishaji kupitia reli.

Inatajwa hiyo njia katika maeneo ya kununua vichwa na mabehewa kwa ajili ya kusafirisha bidhaa kwenda nchi zao ya TRC.

Pia, hali hiyo inatajwa kuhamasisha kampuni kutoka nchi jirani kuwekeza katika treli kuunganishwa na Tanzania, ili kurahishisha usafirishaji, hata unapunguza gharama za usafirishaji kwao, pia kupunguza kasi ya uharibifu wa miundombinu yao ya barabara.

Kijografia, Tanzania ni kiunganishi cha miji mikubwa ya nchi mbalimbali za jirani ikiwamo; majiji Kampala (Uganda), Bujumbura (Burundi), Kigali (Rwanda), Nairobi (Kenya), na Lubumbashi (DRC), ambako kunaguswa na uendeshaji reli ya SGR.

Hapo inatajwa kuongeza mzunguko wa biashara unaokua kwa kasi nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Mtazamo wa mjumuisho wa yote, ndio unapotamka kuwapo mkakati uliopo wa kushirikisha sekta binafsi anaoupigania Rais Dk. Samia, kuendeleza Diplomasia Uchumi.

Hapo kunatajwa ni katika nchi za Afrika Mashariki, jumuiya ya COMESA, yaani Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika, hali Kadhalika kwenye Soko la Pamoja la Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Mahsusi mtendaji huyo mkuu anataja ni pamoja na reli ya SGR inayoendelea kujengwa.

Tayari hatua zake zinatajwa si haba, kwani majaribio ya treni ya mwendokasi kutoka Dar es Salaam, kwenda Morogoro umeshakamilika, kusubiri hatua za uzinduzi wake na safari kuanza.





# Profesa Kitila ataja mwarobaini kudhibiti upotevu wa maji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo amesema katika kukabiliana na suala la upotevu wa maji, kunapaswa kuwekwe kigezo cha kupima utendaji wa wakurugenzi wa mamlaka za maji nchini kwa miezi sita, kabla ya kupewa mkataba.

Amesema hatua zisipochukuliwa kukabiliana na upotevu huo unachangia gharama za uendeshaji kwa mamlaka.

Katika Ripoti ya Utendaji wa Mamlaka hizo kwa Mwaka 2022/23 iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) juzi, inaonesha upotevu wa maji dhidi ya kiwango cha maji kinachozalishwa umeongezeka kutoka asilimia 35.5 mwaka 2021/22 hadi kufikia asilimia 37.2 mwaka 2022/23.

Ripoti hiyo inaonesha kiwango kikubwa cha upotevu wa maji kilichangiwa na mamlaka za maji kuwa na utekelezaji hafifu wa mikakati ya kupunguza upotevu wa maji.

Katika mwaka wa mapitio, mamlaka za maji 10, ambazo ni Kishapu, Maganzo, Busega, Nzega, Kashwasa, Mwanhuzi, Kasulu, Rujewa, Igunga na Kahama zilikuwa na upotevu wa maji chini ya asilimia 20.

Wakati mamlaka za maji 13, ambazo ni Mahenge, Arusha, Mpanda, Vwawa-Mlowo, Makonde, Mpwapwa, Itumba-Isongole, Ifakara, Kiomboi, Rombo, HTM, Ushirombo na MugangoKiabakari zilikuwa na upotevu wa maji wa zaidi ya asilimia 50.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021, mamlaka za maji zinatakiwa kuhakikisha upotevu wa maji hauzidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 17 kati ya 85, ambazo ni DAWASA, Kahama, Moshi, Musoma, Shinyanga, Tanga, Bukoba, Bariadi, Makonde, Maswa, Biharamulo, Bunda, Igunga, Ngara, Nzega, Utete na Busega zilikuwa na mkakati wa kupunguza upotevu wa maji.

Akifungua mkutano wa mapitio ya sekta ya maji ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya maji ya kitaifa ya mwaka 2024, Waziri Mkumbo alisema: "Kwenye mkataba wako kama mkurugenzi wa maji basi tutakupima kwa kiasi gani unashughulikia upotevu wa maji, kwa hiyo tunakupa miezi sita kama kipindi cha uangalizi, tutakudhibitishia kama utakuwa umepunguza asilimia tano ya upotevu wa maji."

Alisema ni vyema kuwekwa kwa kigezo cha kupimwa baada ya miezi sita ya uangalizi kabla ya kupewa mkataba wa nafasi walizoteuliwa ili wapambane kukabiliana na hali hiyo.

"Pia kuwe na kigezo kuwa baada ya muda wa mkataba wao kuisha watapimwa kwa kupunguza upotevu wa maji, wakati Prof. Makame Mbarawa akiwa Waziri wa Maji aliwahi kuweka kigezo cha kuongeza mapato ambapo walifanikiwa mapato."

"Tukiendelea kutowabana bado maji yanayozalishwa yataendelea kupotea kwa kiwango hicho ambacho ni kikubwa. Tunawekeza fedha nyingi hala-fu maji yanapotea haipendezi, Rais (Samia Suluhu Hassan) anawekeza fedha nyingi katika miradi ya maji nchini,"alisema.

Awali, Mratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSSP 11), Remigius Mazigwa alisema licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa programu ya WSSP bado kuna tatizo la utoshelevu wa maji kutokana na mahitaji ya maji na madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Wakati huo huo, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF), Haji Nandule amekabidhi hundi ya Sh. milioni 800 kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda baada ya kuwa mamlaka ya kwanza kukidhi vigezo vya mkopo nafuu unaotolewa kwa ushirikiano na Benki ya Uwekezaji (TIB).

Hivi karibuni akizindua ripoti hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri alisema atazichukulia hatua mamlaka ambazo utendaji wake hauridhishi kwa kuwa na kiwango kikubwa cha upotevu huo na kusuasua kwenye ukusanyaji wa mapato.





Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Mhandisi Yahya Samamba (kushoto), akimkabidhi leseni ya kuongezewa muda wa uchimbaji kwa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu uliopo wilayani Msalala, mkoani Shinyanga kwa Meneja wa Barrick nchini, Melkiory Ngido, katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma jana. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (wa pili kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha. Leseni hiyo mpya iliyotolewa ni ya kipindi cha miaka 27. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBS: Bado kuna tatizo la utumiaji takwimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema bado kuna tatizo la takwimu, kwamba asilimia 40 zinatokana na vyanzo visivyozoeleka na hivyo kushindwa kutumika kwa kukosa uhakika wa ubora wake.

Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu, Utafiti na Shughuli za Kiutakwimu wa NBS, Emilian Karugendo aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya watakwimu yaliyoandaliwa na Chuo cha Takwimu Afrika Mashariki (EASTC) jijini hapa ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuendeleza Takwimu Awamu ya Pili (TSNP).

Alisema takwimu wanazozalisha kupitia vyanzo vya asili yaani utafiti na sensa vinachangia siyo zaidi ya asilimia 60 ya takwimu zinazohitajika kuripoti maendeleo ama utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Alibainisha kuwa maana yake ifikapo mwaka 2030, wanahitaji kuripoti wamefikia wapi kwenye SDGs lakini kuna tatizo la takwimu zinazotoka katika vyanzo ambavyo havijazoeleka.

"Zaidi ya asilimia 40 ya takwimu tulizonazo zinatoka katika vyanzo visivyozoeleka kwa maana kuna changamoto ya takwimu ambazo zinatokana na vyanzo ambavyo havijazoeleka vya takwimu za kiutawala,"alisema.

Alisema takwimu za kiutawala ni zile zinazopatikana kutokana na utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya utendaji na kuwa zipo nyingi katika halmashauri nchini na taarifa hizo zimekuwa hazitumiki kwa sababu hawana uhakika na ubora wake kwa maana ya ukamilifu wa taarifa.

Awali, Makamu Mkuu wa Chuo cha Mipango, Fedha na Utawala wa EASTC, Dk. France Shayo alisema mafunzo hayo yatatolewa kwa wataalam wa takwimu kutoka halmashauri na manispaa zote.

# PPRA yazidi kujitanua, yafungua ofisi kanda tano

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIKA kusogeza huduma kwa wananchi na kusimamia sekta ya ununuzi wa umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeendelea kutanua wigo kwa kufungua ofisi katika kanda tano nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Eliakim Maswi aliyasema hayo jana jijini hapa katika kikao cha wafanyakazi wa mamlaka kilichohudhuriwa na viongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) ngazi ya mkoa.

Alizitaja ofisi hizo ni Kanda ya Ziwa (Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza), Kanda ya Kati (Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora), Kanda ya Kaskazini (Jengo la PSSSF jijini Arusha), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Jengo la NHIF jijini Mbeya) na Kanda ya Kusini (Jengo la PSSSF mjini Mtwara).

Alisema hali hiyo inafanya mamlaka kuwa na ofisi sita za kanda kwa kujumlisha na ofisi ya Kanda ya Pwani iliyopo jengo la Wizara ya Fedha jijini Dar es salaam iliyokuwepo awali

"Naishukuru sana Serikali kwa kuiwezesha mamlaka kusogeza huduma kwa wananchi. Hii ni sehemu ya mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wake. Sasa wananchi hawatakuwa na ulazima wa kuja Dodoma ili wafike PPRA, kila kanda watahudumiwa kikamilifu," alisema Maswi.

Aliongeza kuwa kila Kanda imewezeshwa kuwa na wafanyakazi wa idara zote ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi mahitaji ya wananchi na wadau wa sekta ya ununuzi katika maeneo yao, akisisitiza kuwa wameweka nguvu pia kwenye utoaji wa huduma za Mfumo wa Usimamizi wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST).

Aidha, aliwasihi wafanyakazi wa mamlaka hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kwa kuzingatia uzalendo ili kufanikisha malengo ya serikali ya kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana kwenye ununuzi wa umma.

Mwenyekiti wa TUGHE Mkoa wa Dodoma, Maulid Kipeneku alitoa rai kwa wafanyakazi PPRA kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi, kwa kuzingatia sheria na taratibu.

Aidha, aliwapongeza wafanyakazi hao kwa jinsi wanavyotoa huduma kwa wananchi na kwamba anaamini wafanyakazi hodari watapatikana ndani ya mamlaka hiyo.





## Wanafunzi waeleza faida elimu ya kodi kutolewa shuleni

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Njombe (NJOSS) wamesema kutolewa kwa elimu ya kodi shuleni itawasaidia kutambua umuhimu wa kulipa kodi, sambamba na kuhimizana kudai risiti wakati wanaponunua bidhaa.

Waliyasema hayo wakati wakizungumza na Nipashe baada ya kupata elimu ya mlipa kodi kutoka kwa maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe.

Walisema kupitia elimu hiyo wamefahamu umuhimu wa kodi ambayo imesaidia serikali kuendesha mpango wa elimu bure kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

Mmoja wa wanafunzi hao, Daniel Kasochela alisema elimu ya kodi katika shule yao inatuandaa na kuwapa hamasa ya kuwa walipakodi wazuri hapo baadaye.

"Pia elimu hii itatusaidia kutoa elimu kwa wengine hasa jamii yetu kwamba kuwa kuna umuhimu wa kulipa kodi ili nchi iweze kujiendesha," alisema Kasochela.

Kasochela alisema pia itawasaidia endapo watajiunga na kuwa wafanyabiashara au wajasiriamali kuweza kuchangia pato la taifa ambalo litaongeza uboreshaji wa miundombinu nchini.

Innocent Mwamanyago alisema elimu hiyo imewasaidia kuwa wazalendo sambamba na kujua kwamba kodi wanayotoa hawaitupi badala yake inawarudia kwa kufanyiwa maendeleo.

"Kwanza nikizungumza kama mnufaika wa elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha sita ni elimu ambayo kupitia serikali kodi zake inazokusanya inakuja kuturudishia sisi kama raia wake," alisema Mwamwanyago.

Alisema kulipa kodi ni uzalendo lakini pia kunasaidia kuiwezesha serikali kutimiza majukumu yake kwa wananchi.

Aidha, Joshua Mahenge alisema kuanzishwa kwa chama cha kodi katika shule yao kunasaidia kukumbusha na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kodi.

"Tumepata kujua umuhimu wa kodi hasa sisi ambao ni wanufaika wa elimu bure imetusaidia pia kupata huduma za kijamii ikiwemo afya, barabara na maji kupitia hizi hizi kodi ambazo serikali inakusanya kwa Watanzania," alisema Mahenge.

Ofisa Elimu kwa Mlipa Kodi, Brian Shoo aliwataka wanafunzi hao kudai risiti pindi wanaponunua bidhaa hata kama ni ndogo na kwamba elimu hiyo pia waipeleke kwa wazazi ili kusaidia kutoikosesha serikali mapato.

Ofisa Mkuu wa Uhusiano TRA nchini, Oliver Njunwa alisema lengo la kuanzishwa kwa vyama hivyo katika shule za sekondari ni kusaidia wanafunzi kufahamu umuhimu kulipa kodi ili wao wakaifikishe katika jamii zao kwa sababu kodi ni chanzo kikubwa mapato ya serikali.

# Wananchi wakosa huduma za afya, wafuata gerezani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Isanga jijini Mbeya wamesema wanalazimika kwenda kupata huduma za afya katika Hospitali ya Gereza la Ruanda ama katika kata jirani kutokana na kata hiyo kutokuwa na kituo cha afya ama zahanati.

Waliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Meya wa Jiji la Mbeya, Sheikh DorMohamed Issa iliyokuwa imelenga kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa zahanati katika Mtaa wa Ilolo ambayo ndiyo ya kwanza katika kata hiyo ambayo imefikia hatua ya uezekaji.

Mmoja wa wananchi hao, Syoni Mwakalebela ambaye ni mkazi wa Mtaa wa Igoma A, alisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa kusafiri kwenda kutibiwa kwenye maeneo mengine.

Alisema ujenzi wa zahanati hiyo katika eneo lao utawasaidia kupata matibabu jirani na makazi yao na hivyo kupunguza gharama za usafiri ambazo walikuwa wanazitumia.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kuamua kutujengea zahanati hii maana sasa tutaacha kwenda kutibiwa kule gerezani na Kituo cha Afya cha Ruanda, miaka yote tulikuwa hatuna zahanati wala kituo cha afya," alisema Syoni.

Alisema kitendo cha kukosekana huduma za afya kwenye eneo lao kimekuwa kikiwatesa zaidi wanawake kwa maelezo kuwa wakati mwingine wakishikwa na uchungu usiku wamekuwa wakipata wakati mgumu.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ilolo, Angelo Sanga alisema mbali na kukosa huduma za afya lakini pia kuna miundombinu ya huduma zingine za kijamii ambayo ilikuwa haikuwa katika hali nzuri lakini serikali imeanza kuiboresha.

Alisema katika Shule ya Msingi Isanga vyumba vya madarasa vilikuwa vimechakaa lakini kwa sasa serikali imeanza kukarabati pamoja na kujenga vyoo vya kisasa kwa ajili ya wanafunzi wa shule hiyo.

Vilevile alisema serikali imeanza kukarabati barabara za mitaa ambazo zilikuwa na hali mbaya pamoja na kuanza kujenga baadhi kwa kiwango cha lami.

Alisema ubovu wa miundombinu ya barabara katika maeneo yao ulikuwa unasababisha vyombo vya moto kushindwa kupita hasa magari na bajaji hali iliyokuwa inawafanya watembee kwa miguu mpaka kwenye Barabara ya Mbeya-Chunya.

"Ilikuwa ukitaka kumpeleka mgonjwa hospitalini unashindwa kupata gari kwa sababu wenye magari wanaogopa kuja huku kutokana na ubovu wa barabara, kwa sasa serikali yetu imeanza kutuboreshea barabara hizi," alisema Sanga.

Meya wa Jiji la Mbeya, Sheikh Issa alisema zahanati hiyo ni sehemu ya ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2020 na kwamba inajengwa kwa mapato ya ndani ya halmashauri na mchango wa serikali.

Alisema walianza kutekeleza mradi huo mwaka jana na kwamba mpaka kukamilika kwake itagharimu Sh. milioni 250 ambapo mchango wa serikali kuu ni Sh. milioni 50 ambazo bado hazijaingia.

Aliwataka wakazi wa kata hiyo kuendelea kuvuta subira wakati serikali inaendelea na ujenzi wa mradi huo akieleza kuwa baada ya kukamilisha wataendelea na michakato ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya.



Mkazi wa kijiji cha Mumvwa, kata ya Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, akiwaonyesha wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (ACRI) na Bodi ya Kahawa nchini, wadudu aina ya konokono wanaoshambulia mazao mbalimbali ikiwemo kahawa, walipowatembelea juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Washauri waandishi wa habari kupewa ithibati ya Kiswahili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa Lugha ya Kiswahili nchini wameshauri Baraza la Taifa la Kiswahili (BAKITA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA) kuanza kutoa Ithibati maalumu ya Kiswahili kwa waandishi wa habari.

Aidha wameshauri kuwepo na mkakati endelevu wa utoaji mafunzo ya matumizi sahihi ya Kiswahili kwa waandishi wa habari ili kufanya marekebisho ya makosa katika matumizi ya lugha ambayo yamekuwepo miongoni mwao.

Walitoa maoni hayo juzi wakati wakichangia mijadala mbalimbali kuhusu fursa za ubidhaishaji wa Kiswahili duniani kwenye Kongamano la Nne la Idhaa za Kiswahili ambalo linatarajiwa kuhitimishwa leo.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa cha mkoani Iringa, Dk. Focus Nchimbi alisema waandishi wa habari ni wadau muhimu katika kutangaza na kukuza Kiswahili na kukifanya bidhaa muhimu duniani, hivyo ni muhimu kuwafundisha matumizi sahihi ya lugha hiyo.

"Ikiwa tunataka kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa itakayouzwa duniani ni lazima kwanza turekebishe makosa yaliyopo hasa kwa waandishi wa habari ambao wana mchango mkubwa kueneza lugha hii, watumie lugha kwa ufasaha," alisema Dk.Focus.

Mhadhiri wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM), Dk. Titus Mpemba alisema waandishi wa habari wanapaswa kujengewa uwezo wa kukipa thamani Kiswahili.

Alipendekeza kuwepo kwa mashindano na tuzo mbalimbali za kutambua mchango wa wanahabari wanaofanya vizuri kwenye matumizi sahihi ya Lugha ya Kiswahili ili kuhamasisha wengine kufanya kazi zao kwa kuzingatia matumizi sahihi ya lugha hiyo.

Mwandishi wa Habari, Edda Sanga alisema waandishi na watangazaji wa wamekuwa wakifanya makosa mengi ya Kiswahili, hivyo wataalamu wanapaswa kuyafanyia kazi makosa hayo. Alisema ikiwa waandishi na watangazaji watazingatia matumizi sahihi ya Kiswahili, watakuwa na nafasi kubwa ya kuuza bidhaa hiyo duniani kote kwa kuandaa makala za lugha hiyo na kuziuza kwenye vyombo vya habari vya nje.

Meneja wa Huduma za Utangazaji wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Andrew Kisaka alisema tayari wameanzisha kamati ndogo inayoandaa waraka wa maudhui bora ya Kiswahili kwa kushirikiana na BAKITA, UDSM na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Alisema mamlaka hiyo iko mbioni kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Kiswahili kwa wanahabari nchini, hivyo watazingatia maoni yaliyotolewa na wadau kwa ajili ya kwenda kuyafanyia kazi ili kusaidia vyombo vya habari kukuza Kiswahili.





# Waziri ataka hatua za haraka kunusuru ajali bodaboda

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAMLAKA zinazosimamia usalama wa barabarani hususani waendesha pikipiki (bodaboda) wametakiwa kuchukuwa hatua za kisheria pamoja na kusimamia vyema ajali zinazojitokeza kila siku.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed aliyasema hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya usalama pamoja na wawakilishi wa waendesha bodaboda katika Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi hapo Kisauni Wilaya ya Magharibi "B" Unguja.

Dk. Khalid alisema kuwa ajali za barabarani zimekuwa nyingi kwa sasa hususani kwa waendesha bodaboda hali ambayo kusababisha nguvu ya taifa kupotea kwa wingi.

Aidha, alisema kwamba bodaboda huwapakia watoto zaidi ya wanne jambo ambalo halikubaliki kisheria.

Alisema kuwa watoto chini ya miaka saba akipanda kwenye bodaboda itamlazimu akae na mtu kwa lengo la kumlinda mtoto huyo.

Naye Mwanasheria wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Hassan Vuai alisema kuwa kuna changamoto nyingi ambazo zinazosababishwa na waendesha pikipiki ikiwemo madereva wengi kufanya biashara hiyo bila ya kuwa na leseni pamoja na kutohudhuria kwenye mafunzo ya huduma ya usafirishaji.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Kusini Unguja, Daniel Shillah, alisema kuwa elimu inahitajika kutolewa kwa jamii kwa lengo la kuelewa wajibu wao, kufanya hivyo itaweza kupunguza ajali zinazojitokeza.

Katika kipindi cha mwaka jana ajali 96 zimeripotiwa Zanzibar ikiwemo usafiri wa pikipiki.

# Dk. Mwinyi ataja faida za utoaji vitalu vya mafuta, gesi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema uzinduzi wa duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu vya mafuta na gesi asilia Zanzibar, utafungua na kuharakisha shughuli za utafutaji wa nishati hiyo baharini. Amesema pia utaitangaza Zanzibar kuwa sehemu ya uwekezaji wa mafuta na gesi asilia dunia.

Aliyasema hayo juzi visiwani hapa wakati wa hafla ya uzinduzi wa duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu kwa kampuni za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Dk. Mwinyi aliwahikikishia wawekezaji wote wa sekta ya mafuta na gesi na sekta nyingine za uchumi kwamba, Serikali iko tayari kuwahakikishia mazingira mazuri ya uwekezaji kwa manufaa ya wote.

"Serikali inapenda kuzialika kampuni zote za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi kuweza kushiriki katika duru hii na Serikali ipo tayari kutoa kila aina ya ushirikiano katika kufanikisha jambo hili" alisema.

Dk. Mwinyi alisema shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa upande wa Zanzibar, zilianza miaka ya 1950 wakati Kampuni ya British Petroleum (BP) kwa kushirikiana na Kampuni ya Shell zilipofanya uchunguzi wa kina na kuchimba visima viwili kwa pande zote mbili za Zanzibar.

Alisema shughuli hizo zilikamilika mwaka 1963 na kutoa msingi mkubwa katika kuendeleza shughuli za mafuta na gesi asilia Zanzibar.

"Baada ya Mapinduzi Zanzibar na Muungano wa Tanzania mwaka 1964, shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi zilikua chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo la Petrolii Tanzania (TPDC)" alisema Dk. Mwinyi. Aidha alisema utafiti mbalimbali zilifanyika kwa upande wa nchi kavu na baharini Zanzibar na kusababisha kupatikana kwa vitalu vya Pemba na vitalu nambari 6 hadi 12 na Kisiwa cha Fungu Mbaraka (Kisiwa cha latham).

Hata hivyo alisema hatua mpya ya maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi Zanzibar ilianzishwa mwaka 2015 kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Petroli Namba 21 ya Mwaka 2015 ya Tanzania iliyoiruhusu kila upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusimamia shughuli za mafuta na gesi asilia wenyewe. "Kwa mantiki hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliandaa Sera ya Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2016" alisema.

Dk. Mwinyi alisema sheria hiyo ya mwaka 2016, ilianzisha taasisi za usimamizi wa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia ambazo zilifanyika kati ya mwaka 2017 na 2019.

"Matokeo ya shughuli hizo yameonesha kuwepo kwa miamba na viashiria vyenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi rasilimali za mafuta na gesi asilia hapa Zanzibar"alisema.

Alisema baada ya hatua hiyo, sambamba na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nane ya kutekeleza sera ya uchumi wa buluu, sekta ya mafuta na gesi imewekwa miongoni mwa maeneo makuu ya kipaumbele katika sera ya uchumi wa buluu.

Alisema dhamira ya Serikali katika uchumi wa buluu ni kuimarisha uchumi wa nchi kwa haraka na kuhakikisha upatikanaji wa maendeleo endelevu ya vyanzo vya nishati ya uhakika.

Alisema serikali inaamini kuwa uchumi wa buluu una fursa nyingi za kukuza mipango ya maendeleo ya kiuchumi yenye lengo la kupunguza umasikini na kutengeneza fursa za ajira nchini.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman alisema Sekta ya Uchumi wa Buluu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni miongoni mwa maeneo makuu ya vipaumbele vyake.

Alisema vitalu ambavyo vipo tayari ni nane na wawekezaji wa mafuta na gesi kuazia sasa wameruhusiwa kufanya maombi ili Zanzibar kupata mwekezaji wa uchimbaji na uzalishaji wa nishati hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar, Ali Halilmirza alisema sekta ya mafuta na gesi itafunguwa uchumi katika visiwa hivyo na huo ndiyo utaratibu unaotumika kwa nchi zote za kimataifa katika kutangaza na kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo.

Alisema hatua hiyo ya kutafuta vitalu hivyo ilianza mwaka 2021 mchakato ambao ulikuwa ni mrefu katika kuutangaza, mabadiliko ya sheria ya kuvutia wawekezaji na viwango vya biashara kuvutia zaidi katika mwambao wa Afrika Mashariki.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar, Mikidadi Ali Rashid, alisema uzinduzi huo wa vitalu ni muhimu katika safari ya utafutaji wa nishati hiyo na kupata wawekezaji.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma (katikati mstari wa mbele), Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mwanaidi Ali (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), Dk. Ellen Okoedion, wakishiriki mkutano baina ya Shirika la Kimataifa la masuala ya Wanawake Duniani (UN Women) na Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya wanawake wa Afrika kuhusu usawa wa kijinsia, jijini New York, nchini Marekani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matukio ya udhalilishaji kijinsia Zanzibar yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Februari visiwani Zanzibar yameongezeka kwa asilimia 2.3 na kufikia 175, ikilinganishwa na kipindi cha Januari ambayo yalikuwa 171.

Mtakwimu wa Divisheni za Jinsia na Ajira kutoa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ramla Hassan Pandu aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu takwimu za ukatili na udhalilishaji wa jinsia.

Alisema katika matukio hayo 175 yalioripotiwa matukio ya kubaka yanaongoza ambayo yalikuwa 84 sawa na asilimia 48.0.

Alisema matukio ya kulawiti na kunajisi yalikuwa 11, kuingilia kinyume na maumbile sita, kutorosha 14 kukashifu 23 na shambulio 37.

Alisema katika matukio hayo waathirika ni 176 ambao wengi wao ni watoto kwa asilimia 83.0, wanawake asilimia 13.0 na wanaume asilimia 4.0.

Akizungumzia wilaya zinazoongoza kwa kuwa na matukio mengi yalioripotiwa, alitaja ni Wilaya ya Magharib B Unguja ikiwa na matukio 43, ikifuatiwa na Wilaya ya Mjini na Magharib A Unguja zikiwa na matukio sawa 39.

"Wilaya ya Micheweni Pemba imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio ambayo yalikuwa mawili sawa na asilimia 1.1 ukilinganisha na wilaya nyingine" alisema.

Ramla alisema katika matukio 84 ya ubakaji yaliyoripotiwa matukio matano waathirika ni wanawake na matukio 79 ni wasichana.

Alisema matukio 137 kati ya matukio 175 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 78.3, matukio 33 yapo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 18.9 na matukio matano yapo mahakamani sawa na asilimia 2.9.

Hata hivyo alisema kuwa kuongezeka kwa matukio hayo kunatokana na mwamko wa jamii katika kuripoti matukio hayo katika sehemu husika tofauti na miaka ya nyuma.

TANGAZO

# Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

## 1. POSITION: ADMINISTRATIVE OFFICER II (1 POST)

### 1.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS

- Must be a holder of Bachelor Degree in one of the following fields; Public Administration, Human Resources Management, Human Resources Planning and Management, Manpower Planning, Industrial Relations, Business Administration/Commerce majoring in Human Resources Management or equivalent qualification from recognized institutions or equivalent qualification from recognized institutions

### 1.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES

i. Initiates the updating of a comprehensive, accurate and inventory of all office furniture, fittings and equipment.
ii. Monitors performance of contracted private service providers such as ground maintenance, office cleaning, security guards and catering services to ensure quality of service.
iii. Ensures efficient running of administration transport services at ATCL.
iv. Ensures that machinery and other office equipment are properly maintained.
v. Supervises activities performed by supporting staff such as Drivers, Office Assistants and Messengers.
vi. Keeps a record regarding vehicle maintenance and inspects vehicles' logbooks.
vii. Monitor cleanliness of office premises.
viii. Performs any other official duties as may be assigned by the immediate Supervisor.

## 2. POSITION: HUMAN RESOURCES OFFICER II (1 POST)

### 2.1 MINIMUN ENTRY QUALIFICATIONS

- Must be a holder of Bachelor Degree in one of the following fields; Public Administration, Human Resources Management, Human Resources Planning and Management, Manpower Planning, Industrial Relations, Business Administration/Commerce majoring in Human Resources Management or equivalent qualification from recognized institutions or equivalent qualification from recognized institutions.

### 2.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES

i. Assist in attending staff matters regarding recruitment and selection, confirmation promotions and internal transfers
ii. Assist on preparation of orientation and induction programs
iii. Collect, analyze and keep employment records
iv. Assist in the preparation of performance reports, compile and update personal particulars for employees
v. Assist in preparing training needs assessment.
vi. Assist in interpretation of the scheme of service, staff regulation and various Acts related to employees.
vii. Assist in monitoring of daily staff attendance and recommend solutions to resolve chronic attendance difficulties.
viii. Follow up on all office requirements in liaison with procurement unit.
ix. Prepare staff Leave Roster.
x. Perform any other duty may be assigned by the supervisor.

## 3. POSITION: DRIVER II (4 POSTS)

### 3.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS:

- Must be a holder of Form IV Certificate and a Class "C1 or E" Driving License who has attended Basic Driving Course offered by VETA or any recognized Institution with Driving experience of at least one (1) year without causing accidents. Possession of Trade Test Grade II/Professional Level II in Motor Vehicle Maintenance/Mechanics is an added advantage.

### 3.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES

i. Drive staff towards approved destinations in accordance with traffic regulations.
ii. Take vehicles due for routine maintenance / repair to the appointed service agents.
iii. Undertake minor mechanical repairs.
iv. Maintain log books and records all movement as instructed.
v. Make pre-inspection to the assigned vehicles prior travelling and report mechanical damages / defects.
vi. Certify safety and cleanliness of the vehicle at all times.
vii. Verify that valid documents and permits are acquired prior commencement of any journey.
viii. Perform any other duty may be assigned by the supervisor.

## 4. POSITION: RECEPTIONIST II (1 POST)

### 4.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS

- Holder of a Certificate of Secondary Education with passes in English and Swahili.
- He/she must have attended training in one of the following; Telephone Operation or Front Office Course.
- Must be conversant with basic computer applications.

### 4.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES

i. Answers calling signals
ii. Connects calls within the exchange area
iii. Makes booking calls and searches them as appropriate
iv. Keep safe custody of office property where required;
v. Certify that all office premises are cleaned.
vi. Perform any other official duty may be assigned by the supervisor.

## 5. TERMS AND CONDITIONS:

Ten (10) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

## 6. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

## 7. CLOSING DATES:

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**

***ATCL is an equal opportunity employer. Women are encouraged to apply. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.***

**Date: 22nd March, 2024**

# TABORA UTD YAFUNGUKA KUONDOKA KOCHA WAKE

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Tabora United FC umesema bado Mserbia, Goran Kopunovic, ni kocha wake na amekwenda kwao kutokana na matatizo ya kifamilia aliyopata na si vinginevyo, imefahamika.

**Kumekuwa na tetesi kocha huyo amebwaga manyanya kutokana na kikosi chake kufanya vibaya katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.**

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema Kopunovic ametishia kuondoka katika klabu hiyo kutokana na kupuuzwa kwa ushauri anaoutoa kwa viongozi wa timu hiyo ili kupata matokeo chanya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tabora United, Thabit Kandoro, alisema Kopunovic bado ni mwajiriwa wa klabu hiyo na hata alipoondoka aliacha programu yake ya mazoezi ambayo inasimamiwa vyema hadi hapo atakaporejea.

"Mwalimu alituomba ndani ya hizi siku mbili tatu hatakuwepo nchini kutokana na changamoto zilizo nje ya uwezo wake, sisi tukamwelewa, tukamruhusu, hii yote unayoiona ni programu ya mwalimu aliyoitoa, angekuwa hayupo kwa vyovyote vile, kufukuzwa au kuondoka mwenyewe wachezaji wasingeendelea kufuata aliyoyaacha," alisema Kandoro.

Ofisa huyo alisema kikosi chao kimerejea mazoezini kujiandaa na mechi ya hatua ya 16 bora ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Singida Fountain Gate itakayochezwa Aprili 4, mwaka huu.

"Vijana wamerejea mazoezini kujiandaa na mechi ya Kocha FA pamoja na michezo mingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayofuata, nimekwenda kuwaangalia na nimefarijika, timu imetulia na wanafuata programu ya mwalimu Goran aliyoiacha, na mimi mwenyewe nimeongea naye kwa simu," Kandoro alisema.

Kuhusu kutofanya vyema kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kandoro aliwataka mashabiki wa soka mkoani Tabora kutokata tamaa na amewahakikishia wataona mabadiliko pale ligi itakaporejea.

Timu hiyo inashika nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 21 kibindoni na imecheza michezo 21.




Askofu Mkuu wa Jimbo la Dar es Salaam, Thadeus Rwaachi (katikati), akizungumza kuhusu maandalizi ya mbio za hisani za Pugu Marathon zitakazofanyika Mei, mwaka huu. Kulia ni Mwenyekiti wa Utume wa Wanaume Katoliki (UWAKA), Jimbo Kuu, Amadeus Mosha na Meneja wa Huduma za Kidijitali wa Benki ya Mkombozi, Filemon Tesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Changalawe, Ezra wang'ara Olimpiki

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Ridhaa nchini, Yusuf Changalawe, ametinga hatua ya nusu fainali katika Michezo ya Afrika (All African Games) inayoendelea jijini Accra, Ghana baada ya kumshinda, Maxinillano Bibano, kutoka Equatorial Guinea.

Changalawe aliyekuwa anapigana katika uzito wa Light Heavy aliibuka mshindi baada ya mwamuzi kusimamisha pambano (RSC) kwenye raundi ya kwanza ili kumnusuru na kipigo zaidi mpinzani wake.

Kwa matokeo hayo, Changalawe tayari amejihakikishia kupata medali katika michuano hiyo na sasa atakutana na Pita Kabeji wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kwenye hatua ya nusu fainali.

Mabondia wengine wa Tanzania ambao wametinga nusu fainali ni pamoja na Ezra Mwanjwango (Light) na Mussa Maregesi anayepigana uzito wa Cruiser.

Ezra amejihakikishia medali ya shaba baada ya kupoteza pambano lake dhidi ya Andrew Chilata wa Zambia kwa point za matokeo ya kurejea 5-2 (Bout review) baada ya matokeo ya awali kuwa 3-2.

Tayari timu ya soka ya wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), imerejea nyumbani baada ya kutolewa kwenye hatua ya makundi.



# 'NMB Pesa Haachwi Mtu' yawajaza noti wateja wake

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SHILINGI milioni tano na zawadi nyingine zinazojumisha kofia na mavazi kwa ajili ya mamalishe zimetolewa kwa wateja wa Benki ya NMB waliofungua akaunti ya 'NMB Pesa Haachwi Mtu'.

Kiasi hicho ni sehemu ya zawadi mbalimbali ambazo hutolewa na benki hiyo katika mpango wao wa 'Weka na Ushinde' ambao ulianza kuchezeshwa Februari, mwaka huu na unatarajiwa kukamilika ifikapo Mei, washindi watajinyakulia fedha taslimu Sh. milioni 10, Sh. milioni tatu, pikipiki ya miguu mitatu, friji, mitungi ya gesi na runinga.

Meneja wa NMB, Tawi la Mazengo, jijini hapa, Victor Dilunga, alisema zawadi zilizotolewa ni sehemu ya Sh. milioni 150 ambazo benki hiyo imetenga kwa ajili ya wateja wake katika shindano hilo ambalo jana liliingia hatua ya sita.

Dilunga alisema katika droo hiyo wachezesha kupata washindi wa kila wiki, mwezi na droo kubwa kuliko yote itakuwa ni ile ya mwisho ambayo imebeba kitita kikubwa kuliko vyote tangu walipoanza mpango huo.

"Leo (jana) tumepata washindi 10 ambapo kila mmoja amejinyakulia Sh. 500,000 na tumechezesha kwa uwazi kila mmoja ameshuhudia, urahisi wa kufungua akaunti hii ni mtu kuwa na Sh. 1,000 na kitambulisho cha NIDA au namba yake tu," alisema Dilunga.

Meneja huyo alisema baada ya kufungua akaunti hiyo, mteja anapaswa kuweka Sh. 50,000 na baada ya hapo moja kwa moja atakuwa ameingia katika droo hiyo ambayo inamwezesha kushindania zawadi ya Sh. milioni 150 zilizotengwa kwenye shindano zima.

Ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT), Ibrahimu Sikana, alisema washindi wanaopatikana kupitia mashindano mbalimbali ndani ya NMB wako kihalali kwa kuwa benki hiyo inafuata masharti na sheria za michezo ya kubahatisha kila inapochezesha droo zake.

Sikana aliipongeza benki hiyo kwa kufuata taratibu na kanuni za uchezeshaji michezo ya kubahatisha na kutaka taasisi nyingine zifuate au kuiga namna wanavyofanya NMB kwa sababu wanasaidia kuondoa malalamiko na manung'uniko kwa wanaokosa.

Alisisitiza NMB itaendelea na mfumo uliopo kwa sasa ili waendelee kuaminika, akisema ndio njia pekee inayowapa heshima ya kuaminiwa na taasisi kubwa kwenye matunzo ya fedha za Watanzania.

Meneja Mauzo wa NMB Makao Makuu, Janeth Nyamko, alisisitiza wananchi waendelee kuiamini benki hiyo ambayo imejipambanua kwa kufanya mambo makubwa yenye tija kwa wananchi na mara nyingine imekuwa sehemu ya kuwapa faraja Watanzania.

Nyamko aliongeza awamu ijayo droo itachezeshwa kwenye Tawi la Wami lililoko mjini Morogoro na huo ni utaratibu waliojiwekea wakati michezo hiyo inachezeshwa kwa mzunguko ikihusisha matawi ya nchi nzima.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GALLAGHER KUTUA SPURS

TOTTENHAM Hotspur inajiandaa kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 24, ambaye mkataba wake unamalizika 2025. ***(Teamtalk)***

### ADARABIOYO AGEUKA LULU

LIVERPOOL, Tottenham Hotspur na AC Milan ni miongoni mwa klabu zinazomhitaji mlinzi wa Fulham, Tosin Adarabioyo, mwenye umri wa miaka 26, hata hivyo Fullham wanataka kumpa mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City mkataba mpya. ***(Standard)***

### RAPHINHA HAKIJAELEWEKA

TOTTENHAM Hotspur pia inavutiwa na winga wa Barcelona na Brazil, Raphinha, 27, ambaye mustakabali wake katika klabu hiyo ya LaLiga hauko wazi. ***(Sport)***

### MURILLO SOKONI ENGLAND

LIVERPOOL, Arsenal na Chelsea ni miongoni mwa klabu zinazohitaji kumnunua beki wa Nottingham Forest ambaye ni raia wa Brazil, Murillo, 21. ***(Mail)***

### MAINOO, UNITED MAMBO SAFI

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Kobbie Mainoo, 18, anakaribia kusaini mkataba mpya na Mashetani Wekundu hao. ***(HITC)***

### SILVA KUREJEA FLUMINENSE

MLINZI wa Brazil, Thiago Silva, 39, anawasiliana na klabu yake ya zamani ya Fluminense huku akitarajiwa kurejea nyumbani, mkataba wake na Chelsea utakapokamilika mwishoni mwa msimu joto. ***(Sun)***

### POTTER, O'NEIL WATAJWA

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe, Kocha wa zamani wa Chelsea, Graham Potter na Gary O'Neil wa Wolves wote wanaweza kuwa katika kinyang'anyiro cha kuwania kibarua cha kuinoa England iwapo Gareth Southgate ataondoka kwenda Manchester United. ***(Mirror)***

### MOURINHO KUMRITHI TUCHEL

KLABU ya Bayern Munich inaweza kumgeukia Jose Mourinho, ambaye hana kazi baada ya kutimuliwa Roma kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel anayeondoka ikiwa hawataweza kumpata, Xabi Alonso, anayelengwa. ***(Mirror)***

### CONTE ANUKIA BAYERN

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Antonio Conte, pia anasakwa na Bayern Munich ya Ujerumani. ***(Le Repubblica)***

### LEEDS KUMBAKISHA GRAY

LEEDS United iko tayari kumpa kiungo, Archie Gray, mwenye umri wa miaka 18, mkataba ulioboreshwa katika msimu wa joto huku kukiwa na klabu sita kubwa za Ligi Kuu England zinazotaka kumnunua nyota huyo. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ROBINHO AHUKUMIWA KIFUNGO MIAKA TISA

## Mshambuliaji huyo akata rufaa na amesisitiza alikuwa...

**BRASILIA,** Brazil

MAJAJI katika Mahakama ya Brazil wameunga mkono hukumu ya Mahakama ya Italia ya ubakaji kwa mshambuliaji wa zamani wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Brazil, Robinho, na kuongeza lazima atumike kifungo cha miaka tisa jela.

**Majaji wa mahakama ya juu zaidi ya Brazil walipiga kura 9 kwa 2 kuthibitisha hukumu ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid na Manchester City.**

Robinho mwenye umri wa miaka 40 alihukumiwa Italia kifungo cha miaka tisa jela kwa kushiriki katika kundi la unyanyasaji wa kingono mwaka 2013 alipokuwa akiichezea AC Milan.

Brazil haiwakabidhi raia wake kwa nchi nyingine kutumikia kifungo, hivyo ikaifanya Italia kutafuta kifungo katika taifa lake.

Uamuzi huo uliamuliwa na mahakama ya juu zaidi ya Brazil yenye jopo la majaji 15 katika mji mkuu Brasilia na kumtaka Robinho kutumikia kifungo hicho.

Wakili wa Robinho, José Eduardo Rangel de Alckim, alisema atakata rufaa dhidi ya uamuzi huo katika mahakama ya juu ya Brazil na ataomba mchezaji huyo akae nje ya gereza wakati wa mchakato wa kukata rufaa.

"Robinho yupo na yuko tayari kufika wakati wowote mbele ya majaji na akifika hapo atatii. Hatapinga," alisema Alckim.

"Wasiwasi wetu wa kwanza ni kusitisha agizo la kukamatwa mara moja. Tutaomba hukumu hiyo itekelezwe baada ya uamuzi wa rufaa kufanywa."

Jaji wa kwanza kupiga kura, Francisco Falcão, alisema Robinho anafaa kutumikia kifungo chake Brazil.

Aliongeza mchezaji huyo wa zamani hawezi kuachwa bila kuadhibiwa na msuguano wa kidiplomasia kati ya Brazil na Italia unaweza kutokea iwapo adhabu hiyo haitatolewa.

"Hakuna kikwazo kuthibitisha utekelezaji wa hukumu yake. Ilithibitishwa na mahakama ya Milan ambayo ndiyo mamlaka yenye uwezo katika kesi hii," aliongeza Falcão.

"Hukumu ni ya mwisho. Mshtakiwa hakushtakiwa bila kuwapo Italia, alikuwa na uwakilishi."

Robinho anaishi Santos, nje ya Sao Paulo na hati yake ya kusafiria inashikiliwa na Mamlaka ya Brazil tangu Machi, mwaka jana.

Ameendelea kukana kosa lolote na kusisitiza mahusiano yake ya kimapenzi na mwanamke huyo katika baa ya Milan yalikuwa ya maelewano.

## HABARI MICHEZO



# BAYERN YATOA OFA YA MWISHO KWA DAVIES

**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Max Eberl, amesema klabu hiyo imetoa ofa ya mwisho kwa mlinzi wa kushoto wa Canada, Alphonso Davies, ili kuongeza mkataba wake huku kukiwa na taarifa za kutakiwa Real Madrid.

"Naweza kusema tulimpa Alphonso ofa thabiti na ya shukrani," alisema Eberl akiliambia jarida la Sport Bild Jumatano iliyopita.

"Wakati fulani maishani lazima useme ndio au hapana."

Mkataba wa Davies na Bayern unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, kumaanisha klabu hiyo ya Bavaria inaweza kumpoteza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ifikapo mwakani kwa uhamisho wa bure.

Ripoti za vyombo vya habari vya Hispania zinasema, Davies tayari amefikia makubaliano na Real Madrid kuhusu uhamisho huo, lakini Eberl alisema viongozi hao wa LaLiga hawajawasiliana nao. Bayern Munich bado wanaweza kuamuru ada ya uhamisho ikiwa Davies ataondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

"Hakuna klabu inayotaka kupoteza wachezaji bure," alisema Eberl mwezi uliopita.

Vyanzo vimeiambia ESPN wakati Madrid wakiendelea kumtaka Davies, hawako tayari kulipa zaidi ya euro milioni 40 ili kumsajili msimu huu wa joto na wako tayari kungoja mwaka mwingine kupata huduma yake kwa uhamisho wa bure.

Nia ya Davies ni kujiunga na Madrid, vyanzo viliongeza. Davies, ambaye amefunga mabao 15 katika mechi 45 alizoichezea Canada, amecheza mechi 127 za Bundesliga akiwa na Bayern.

Davies ambaye ni raia wa Canada aliyezaliwa nchini Ghana, alijiunga na Bayern Januari mwaka, 2019 baada ya klabu hiyo kukubaliana uhamisho wa dola milioni 22 na Vancouver Whitecaps mwaka mmoja kabla ya mchezaji huyo wakati huo akiwa na umri wa miaka 17.

# Alves aachiwa huru kwa dhamana

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa zamani wa Brazil, Dani Alves, ameachiwa kwa dhamana ya euro milioni moja baada ya kukata rufaa, Mahakama ya Barcelona nchini Hispania imetangaza.

Alves mwenye umri wa miaka 40, alipatikana na hatia ya unyanyasaji wa kijinsia mwezi uliopita na kuhukumiwa miaka minne na nusu jela, ambayo tayari alikuwa ametumikia zaidi ya mwaka mmoja.

Masharti ya kuachiwa kwa Alves ni pamoja na kutakiwa kukabidhi hati zake za kusafiria kwa Mamlaka ya Brazil na Hispania, pamoja na kuweka dhamana, na haruhusiwi kuondoka nchini humo.

Pia hawezi kufika umbali wa mita 1,000 kutoka kwa mwathiriwa au kujaribu kuwasiliana naye, na lazima aripoti mahakamani kila wiki.

Bado ana makazi jijini Barcelona.

Shirika la Habari la Hispania (EFE), liliripoti dhamana hiyo imekamilika juzi na jana Alves alitoka gerezani.

Pande zote zinazohusika, utetezi, timu ya wanasheria ya mwathiriwa na upande wa mashtaka -- wana siku tatu za kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo.

Ester García, wakili wa mwathiriwa, alielezea kusikitishwa kwake na uamuzi huo kwa RAC1 baada ya kutoka mahakamani.

"Kwa kweli sijaridhika na uamuzi huu," alisema. "Tutakata rufaa kwa sababu tunaamini haiko kwa mujibu wa sheria.

"Haki inatendeka kwa matajiri. Ni kashfa wanamwachia mtu kwa sababu wanaweza kupata euro milioni moja kwa muda mfupi."





# Silva asubiriwa Fluminense

**JIO DE JANEIRO,** Brazil

MKURUGENZI wa Michezo wa Fluminense, Fred, amekiri Thiago Silva bado ni 'ndoto' ya kusajiliwa na klabu hiyo na wanatumani kumwona akirejea Brazil wakati mkataba wake na Chelsea utakapomalizika.

Miamba hao wa Brazil wameweka wazi nia yao ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, ambaye mkataba wake pale Stamford Bridge unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Beki huyo wa kati amekuwa akiwasiliana mara kwa mara na klabu hiyo na anazungumza na rais kila wiki.

Anaweza kurejea katika klabu yake ya nyumbani, ambako alicheza kwa misimu miwili na nusu kati ya 2006 na 2009.

Akizungumza na ESPN Brasil, Fred alisema: "Thiago Silva imekuwa ndoto yetu kwa muda mrefu, rais huzungumza naye karibu kila wiki.

"Thiago ana mkataba kule England, tunamlenga, mimi binafsi ni rafiki yangu, ni shabiki mkubwa wa tabia yake, anastahili kila la kheri, anajua hapa milango iko wazi kwake kurudi.

"Tunapaswa kuwa makini ili tusimpe presha Thiago. Mashabiki wanampenda Thiago, tunampenda Thiago na Thiago anaipenda Fluminense. Siku moja ni jambo lisiloepukika, litatokea, ni matakwa ya wachezaji, matakwa ya klabu na tunatumani itatokea hivi karibuni."

The Blues wanaonekana kutafuta mabeki wa kati kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto. Leny Yoro wa Lille bado anavutiwa na Stamford Bridge, ingawa ripoti zinadai PSG na Real Madrid pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18.

# Benchikha afurahia kambi Z'bar

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema alichagua kambi ya timu yake iwe Zanzibar kwa sababu ya wachezaji wake kupata utulivu na nafasi bora ya kufanya mazoezi kuelekea mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayochezwa Machi 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Benchikha alisema kambi ya Zanzibar inawasaidia kufanya mazoezi asubuhi na usiku, ambao ndio muda watacheza mechi hiyo ya kimataifa na kwa kufanya hivyo wachezaji wake watazoea mazingira hayo.

Kocha huyo alisema mazoezi anayowapa ni ya kujiandaa kukabiliana na timu ngumu ya Al Ahly, mbali na mbinu za kiufundi pia anawaandaa nyota wake kuwa katika hali ya utimamu wa mwili wa hali ya juu ili kuhimili mikiki mikiki ya Wamisri hao ambao wana historia nzuri katika michuano hiyo.

"Tunahitaji kufanya mazoezi mara mbili kwa siku, asubuhi na usiku ili kutengeneza timu ambayo itakwenda kutoa ushindani kwa Al Ahly, nilihitaji kufanya mazoezi muda wa usiku, muda ambao mechi yetu na Al Ahly utachezwa ili wachezaji wazoee mazingira hayo, pia huku (Zanzibar) kuna mazingira tulivu zaidi ambayo yatafanya wachezaji wetu kupumzika na akili yao kujielekeza kwenye mchezo husika," alisema Benchikha.



Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema muda wa mechi hiyo hupangwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na si timu mwenyeji kama ambavyo wadau walitaka mchezo huo ufanyike kuanzia saa 10:00 jioni.

"Wengi walitamani mechi ipigwe mchana kwa ajili ya kuwachosha na joto, lakini mechi hizi zinapangwa na watu wengi na kwa maslahi ya wengi ikiwamo haki ya matangazo, lakini pia CAF wanaangalia ustawi wa timu zote mbili.

Tukumbuke pia kuwa tupo katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, maslahi mapana ya imani ya watu wote yamezingatiwa na mechi zote zimepangwa kwenye muda huo," alisema Ahmed.

# PRODUCER WA DITTO ATOA USHAHIDI MAHAKAMA KUU

**Na Mwandiahi Wetu**

MTAYARISHAJI wa muziki, Emmanuel Maungu, aliyetengeneza audio ya kibao kiitwacho Nchi Yangu cha msanii, Dotto Bernard maarufu Ditto, ametoa ushahidi wake akieleza Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam namna alivyotengeneza wimbo huo mwaka 2017.

Maungu ni shahidi wa pili kati ya watano katika kesi ya Ditto dhidi ya MultiChoice Tanzania Limited anayedai kampuni hiyo imetumia kibao chake kwenye matangazo yao ya biashara kipindi cha Kampeni ya fainali za Kombe la Afrika (AFCON 2019) bila ridhaa yake.

Ditto alifungua kesi akiiomba mahakama iamuru MultChoice Tanzania imlipe fidia ya Sh. bilioni sita kwa kutumia wimbo wake katika matangazo yao ya biashara bila ridhaa yake.

**Pia ameiomba mahakama iamuru alipwe Sh. milioni 200 kutokana na madhara ya jumla, pia alipwe riba ya asilimia 25 tangu siku alipofungua shauri hilo.**

Jana, kesi hiyo iliendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa Ditto mbele ya jaji, Salma Maghimbi.

Producer wa Wimbo huo, Emmanuel Maungu alieleza Mahakama kwamba aliutengeneza wimbo huo mwaka 2017 na alipigiwa simu na Ditto mwaka 2019 kumuuliza endapo yeye (Maungu) ndiye alitoa idhini kwa DSTV kuutumia kwenye matangazo yao.

Akitoa ushahidi wake wa maandishi, alidai alimwambia Ditto sio yeye ndipo akamtumia links kuona walivyoutumia katika matangazo hayo.

Alisema, alianza kutengeneza wimbo wa Nchi Yangu uliombwa na Ditto pekee, kisha akafanya remix ya wimbo huo huo wa Ditto na kushirikishwa wasanii wengine baadhi baada ya Ditto kuombwa ifanyike Remix kwa ajili ya Tamasha la Urithi.

Baada ya kutoa ushahidi wake, Wakili wa DSTV, Thomas Mathias alimuuliza shahidi huyo.

**Wakili:** Nikisema wewe ndiye uliyeingiza biti kwenye wimbo wa Nchi Yangu niko sahihi?

**Shahidi:** Niliingiza sauti

**Wakili:** Unafahamu masuala ya haki miliki?

**Shahidi:** Nazijua za kwangu kama producer

**Wakili:** Tutajie haki kadhaa kama producer

**Shahidi:** Ni kuwa na umiliki sehemu ya muziki nilioingiza

**Wakili:** Unataka kuiambia Mahakama katika wimbo wa Nchi Yangu una haki?

**Shahidi:** Hayo ni makubaliano yangu na Ditto.

Wakili mwingine wa DSTV, alimuuliza shahidi

**Wakili:** Nitakuwa niko sahihi kwamba ulisema wimbo huu una version mbili?

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:** Ni upi ulitumika na Dstv?

**Shahidi:** Nchi yangu version ya pili ulitumika

**Wakili:** Hiyo iliimbwa na nani?

**Shahidi:** Uliimbwa na Ditto kwa kushirikiana na wasanii wengine.

Kesi hiyo itaendelea tena leo katika mahakama hiyo.



Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Dotto Bernard 'Ditto' (mwenye kofia) akiingia katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kwa ajili ya kusikiliza kesi yake ya madai dhidi ya Kampuni ya MultiChoice Tanzania jijini jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga yawatuliza presha mashabiki*

INATOKA UKURASA 24

wanatarajia kuwasili nchini Machi 28, mwaka huu na waamuzi watakaosimamia mechi hiyo wanatoka Misri.

"Tunatambua huu ni mchezo mgumu sana dhidi ya Mamelodi Sundowns lakini tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri ya ushindi hapa nyumbani. Wote tunakubaliana mechi ya Mamelodi Sundowns ni kubwa zaidi katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika," Kamwe aliongeza.

Alitaka kiingilio katika eneo la VIP A kitakuwa ni Sh. 30,000 wakati VIP B ni Sh. 20,000 huku mashabiki watakaokata tiketi za kukaa eneo la VIP C , 10,000 na mzunguko utakuwa bure," alisema Kamwe.

Alisema pia wataendelea na utaratibu wao wa kuipa jina la mchezaji mmoja siku ya mchezo huo na wataweka wazi wiki ijayo ni nyota gani atapewa mechi hiyo.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, mwaka jana walicheza fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na kufungwa na USM Alger ya Algeria.

Hata hivyo Yanga itashu-

# VAR kutumika Ligi Kuu Bara

INATOKA UKURASA 24

nyingine zichezwe kavu.

Alieleza kanuni zitakazotungwa ndizo zitatoa mwongozo kwa VAR hizo mbili zitumike vipi, lakini kwa anavyoona kwa kiasi kikubwa zinaweza kutumika katika michezo inayohusu Simba na Yanga pale zinapokuwa kwenye viwanja viwili tofauti.

"Mara nyingi mechi zinazotusumbua ni zile ambazo wanacheza hawa wakubwa (Simba na Yanga), wanashindana wenyewe, kila mmoja anaweka watu wake kwa ajili ya kurekodi makosa ya waamuzi yanayomnufaisha mwenzake na kurusha, huwezi kuona mechi ya Coastal na Ihefu makosa ya waamuzi yanarushwa na kujadiliwa katika mitandao ya kijamii," aliongeza Karia.

Alisema imefika wakati wa kuwalinda waamuzi wa Kitanzania ambao wanaheshima katika mashindano ya kimataifa yanayosimamiwa na CAF kwa kuwaletea VAR.

"Wenzetu wanawalinda sana marefa wao, wanafanya mambo ya ajabu sana, waamuzi ni binadamu, wengine wanapitiwa, wengine wanafanya makusudi, lakini wanalindwa, pia wanasaidia wa VAR, kwetu likifanyika tu tunawarushia dunia nzima," alisema kiongozi huyo.

# Michezo



Ijumaa Machi 22, 2024

**Nipashe**

Robinho ahukumiwa kifungo miaka 9 UKURASA 22



Kiungo wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mudathir Yahya, akifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Bulgaria itakayochezwa leo kwenye mji wa Baku nchini Azerbaijan. **PICHA: TFF**

## VAR kutumika Ligi Kuu Bara 2024/25

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, amesema vifaa vya kiteknolojia kwa ajili ya kuwasaidia waamuzi (VAR), vitaanza kutumika rasmi katika mechi za Ligi Kuu Bara kuanzia msimu ujao.

Karia pia amekaribisha maoni ya kanuni ya kuzikata timu pointi ambazo wachezaji au mashabiki wake watakaonekana kufanya vitendo vinavyoashiria ushirikina na kuingia uwanjani wakati mechi inaendelea.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Karia alisema tayari wameshapokea nyaraka kutoka katika Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa ajili ya kupokea vifaa vya VAR, lakini kabla ya hapo kutakuwa na mafunzo kwa waamuzi ya namna ya kuvitumia.

"Ndiyo, tayari CAF wametusaidia wanatuletea VAR katika ule mpango wake wa kusaidia 'zone' zake, lakini kwanza kutakuwa na mafunzo ya jinsi ya kuitumia, tumeshapokea nyaraka, na tuko katika mchakato wa kuomba kusamehewa kodi serikalini kabla kupokea ule mzigo wenyewe wa vifaa kabla ya kufungwa," alisema Karia.

Mbali na VAR itakayoletwa kwa msaada wa CAF, Karia alisema wadhamini wao waliochukua jukumu la kuonyesha mpira kwenye televisheni nao wamemwahidi kununua mashine inayotembea, hivyo Tanzania kutakuwa na VAR mbili, ingawa alisema inabidi kanuni za ligi zirekebishwe kwani baadhi ya mechi zitakuwa zinachezwa bila kifaa hicho.

Rais huyo alisema VAR inayotembea itaanza kufanyiwa majaribio katika mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yatakayofanyika kuanzia Juni 29 hadi Julai 14, mwaka huu huko Zanzibar.

"Wadhamini wetu wanaoonyesha mpira kwenye televisheni nao wamesema watanunua VAR inayotembea, yenyewe itakuwa inahamishika, inaweza kuwa uwanja huu leo, kesho ikaenda kutumika kwenye uwanja mwingine, ile ya CAF yenyewe itafungwa kwenye Uwanja wa Mkapa, kwa hiyo itatumika hapo tu na hii ya kuhamishika itakwenda Tanga au Morogoro," Karia alisema.

Aliongeza lazima zitengeneze kanuni kwa sababu haiwezekani katika mechi nane, ni michezo mwili tu ndizo iwe na VAR na mechi

INAENDELEA UKURASA 23

# *Yanga yatuliza presha mashabiki*

## ●●● Ni kuhusiana na afya ya nyota wake, Aucho naye kimeeleweka...

**Na Saada Akida**

HABARI njema katika kambi ya Yanga ni kuimarika kwa afya za wachezaji wake nyota waliokuwa majeruhi ambao ni Pacome Zouazoua, Yao Kouoassi na Khalid Aucho, kwa ajili ya kujumuishwa katika mpango wa mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundwons kutoka Afrika Kusini, imeelezwa.

Yanga inatarajia kuwakaribisha Mamelodi Sundowns katika mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali itakayochezwa Machi 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na marudiano yakifanyika Aprili 5, mwaka huu huko Afrika Kusini.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema mazoezi ya timu yao yanayohusisha nyota ambao hawajaitwa katika vikosi vya timu za taifa yanaendelea vyema na tayari wamepokea taarifa kuhusiana na Yao ambaye hali yake imeimarika.**

Kamwe alisema nyota huyo kwa sasa ana asilimia 50 ya kucheza mchezo huo wa kimataifa na wanaamini huenda hali ikawa bora zaidi kutokana na matibabu sahihi aliyopatiwa.

Alisema kwa upande wa Pacome, uongozi unasubiri kupokea ripoti kutoka kwa madaktari wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast iliyoweka kambi yake Ufaransa, mshambuliaji wao akiwa ameitwa kuitumikia nchi yake.

"Pacome bado hajawa timamu lakini daktari wa Timu ya Ivory Coast amemwomba mchezaji huyo ili kuona vipi anaweza kusaidia, taarifa zaidi zitatolewa baada ya vipimo kutoka huku na vya huko kujumuishwa, taarifa pia ya daktari wa Yanga itaeleza juu ya ukubwa wa jeraha.

Kuhusu Khalid (Aucho) anaendelea kuimarika na yupo katika wiki ya pili, naye ripoti ya daktari itatoa majibu juu ya nyota huyo ataanza lini mazoezi ya pamoja na Kibwana (Shomari) ataanza mazoezi Jumatatu hii, Zawadi (Mauya) yeye ameanza mazoezi pamoja na wachezaji wengine kuelekea mechi yetu ya Jumamosi," alisema Kamwe.

Aliongeza ushindani na kiu ya wachezaji kufanya vizuri katika mechi hiyo ni mkubwa na hali hiyo inawapa matumaini ya kusonga mbele kwenye mashindano hayo.

Alisema Mamelodi Sundowns

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >